# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA MBUNGE, JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

# UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2015-2020)

## *(TAARIFA YA JANUARI 2016 - JUNI 2019)*

**JULAI 7, 2019**

# YALIYOMO

YALIYOMO ............................................................................1
1. UTANGULIZI.........................................................................5
2. UONGOZI NA MAWASILIANO JIMBONI.......................6
2.1 ZIARA ZA VIJIJINI ZA MBUNGE WA JIMBO ...............6
2.2 WASAIDIZI WA MBUNGE WA JIMBO ..........................7
2.3 MABARAZA YA WAZEE ................................................7
2.4 TOVUTI YA JIMBO ..........................................................8
2.5 REDIO YA MTANDAONI (ONLINE RADIO) ................9
3. HUDUMA ZA JAMII .......................................................10
3.1 SEKTA YA ELIMU ...........................................................10
3.1.1 UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA..................10
3.1.2 MICHANGO YA MBUNGE KWENYE UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA........................................11
3.1.3 MICHANGO YA FEDHA ZA SERIKALI .....................13
3.1.4 MICHANGO YA MFUKO WA JIMBO .........................14
3.1.5 UJENZI WA SHULE SHIKIZI........................................17
3.1.6 MICHANGO YA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGOs).......................................................18
3.1.6.1 PROJECT CONCERN INTERNATIONAL (PCI)..........18
3.1.6.2 EDUCATION QUALITY IMPROVEMENT PROGRAMME (EQUIP)...............................................19
3.1.6.3 EDUCATION PROGRAMME FOR RESULTS (EP4R) 20
3.1.6.4 BMZ .................................................................................21
3.1.7 UGAWAJI WA MADAWATI KWENYE SHULE

ZA MSINGI........................................................23
3.1.8 UGAWAJI WA VITABU VYA SAYANSI NA KIINGEREZA........................................................24
3.1.8.1 MGAO AWAMU YA KWANZA ........................................24
3.1.8.2 MGAO AWAMU YA PILI........................................25
3.1.8.3 MGAO AWAMU YA TATU ........................................26
3.1.8.4 MGAO AWAMU YA NNE........................................27
3.2 SEKTA YA AFYA........................................28
3.2.1 VITUO VYA AFYA ........................................29
3.2.2 KITUO CHA AFYA MURANGI ........................................29
3.2.3 KITUO CHA AFYA MUGANGO ........................................32
3.2.4 KITUO CHA AFYA NYAMBONO........................................32
3.2.5 ZAHANATI ZA SERIKALI ........................................33
3.2.6 ZAHANATI ZINAZOTOA HUDUMA ZA AFYA ........33
3.2.6.1 MICHANGO MINGINE YA MBUNGE WA JIMBO ....35
3.2.7 ZAHANATI BINAFSI........................................36
3.2.8 ZAHANATI MPYA ZINAZOJENGWA NA WANAVIJIJI........................................37
3.2.9 UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA ........................38
3.2.10 MATIBABU KUTOKA KWA MADAKTARI BINGWA WA CHINA ........................................39
3.2.11 MAGARI YA KUBEBEA WAGONJWA (AMBULANCES)........................................41
3.2.12 MICHANGO YA MASHIRIKA YA UMMA ..................44
4. HUDUMA ZA KIUCHUMI ........................................44
4.1 SEKTA YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI................44
4.1.1 KILIMO........................................45
4.1.2 KILIMO CHA UMWAGILIAJI ........................................45

4.1.3 MRADI WA BONDE LA BUGWEMA .......................... 46
4.1.4 KILIMO CHA ALIZETI ................................................ 47
4.1.4.1 MITAMBO YA KUKAMUA MBEGU ZA ALIZETI .... 49
4.1.5 KILIMO CHA MIHOGO ............................................. 50
4.1.6 KILIMO CHA MTAMA ................................................ 51
4.1.7 UBORESHAJI WA ZANA ZA KILIMO ........................ 52
4.2 UVUVI .......................................................................... 53
4.3 UFUGAJI ....................................................................... 54
5. MIRADI YA MAJI, UMEME NA BARABARA ........... 54
5.1 MIRADI YA MAJI ......................................................... 54
5.1.1 MIRADI YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 ............................................................ 54
5.1.2 MIRADI YA MAJI AMBAYO USANIFU UMEKAMILIKA ............................................................ 58
5.2 MRADI WA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI (REA) 58
5.3 MIRADI YA BARABARA ............................................. 60
5.3.1 UJENZI WA BARABARA YA LAMI (TANROADS) .. 60
5.3.2 MATENGENEZO YA BARABARA (TANROADS)..... 60
5.3.3 BARABARA VIJIJINI (TARURA)................................ 61
6. USAFIRI JIMBONI (MAGARI YA MBUNGE) ............ 62
7. UTUNZAJI WA MAZINGIRA ...................................... 63
8. MICHEZO NA UTAMADUNI ...................................... 64
8.1 KUDUMISHA NA KUKUZA UTAMADUNI ............... 64
8.2 MPIRA WA MIGUU ..................................................... 67
9. USHIRIKI KWENYE MASUALA YA KIJAMII........... 69
10. KUSHIRIKIANA NA MADHEHEBU YA DINI............ 72
11. KUWAJENGEA VIJANA UWEZO NA UJUZI ............ 74
12. MICHANGO YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI

ZA CHAMA ........................................................................75
12.1 SEKRETARIETI YA WILAYA ......................................75
12.2 MICHANGO YA VIKAO VYA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE ..............................................................77
12.3 ZIARA ZA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE ..................78
12.4 CHAGUZI ZA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE............78
12.5. SHEREHE ZA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE............79
13. WAZALIWA WA VIJIJI VYA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI.........................................................81
14. KUJADILI NA KUTATHMINI MAENDELEO YA JIMBO ..........................................................................83
15. HITIMISHO ....................................................................85
16. SHUKRANI .....................................................................86
17. KIAMBATANISHO NAMBA I .....................................89

# 1. UTANGULIZI

Jimbo la Musoma Vijijini lenye Jumla ya Kata 21, Vijiji 68, Vitongoji 374 na Wakazi takriban Laki Tatu (300,000) lina Vipaumbele Vikuu Vitano (5) ambavyo ni (i) Elimu, (ii) Afya, (iii) Kilimo (Uvuvi na Ufugaji), (iv) Mazingira, na (v) Michezo na Utamaduni. Haya yote yamo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 – 2020. Maji, Umeme, Barabara, Vyombo vya Usafirishaji na Mawasiliano ni nyenzo muhimu zinazotumika kufanikisha utekelezaji wa Miradi ya Vipaumbele hivyo vitano. Ukuaji na Uimarikaji wa Uchumi na Ustawi wa Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini, ndilo lengo kuu la Vipaumbele hivyo vitano.

Miradi ya Maendeleo ya Vipaumbele hivyo vitano na nyenzo zake inabuniwa na Wanavijiji kwa kushirikiana na Viongozi wao tokea ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Miradi yote inayobuniwa na kutekelezwa inafuata utaratibu wa Serikali na Serikali huwa inaunga mkono Juhudi za Wanavijiji kwenye Vijiji vyote 68 vya Jimbo la Musoma Vijijini. Mbunge wa Jimbo, Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo anashirikiana kwa karibu sana na Wananchi na Viongozi wao wa ngazi mbalimbali kwenye Utekelezaji wa Miradi iliyopendekezwa na Wananchi wenyewe. Vilevile, Mbunge huyu wa Jimbo anashirikiana kwa karibu sana na Serikali na Viongozi wake wa ngazi zote kwenye Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini.

Taarifa hii inaeleza Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020) kwenye Jimbo la Musoma Vijijini kwa muda wa Miaka

Mitatu na Nusu (Januari 2016 – Juni 2019). Vilevile, Taarifa hii inaonesha Michango mingi na mikubwa iliyotolewa na Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwenye Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini. Kwa ujumla Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020) inatekelezwa kwa Mafanikio Makubwa sana na hii inathibitisha jinsi ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt John Pombe Joseph Magufuli inavyowaletea Wananchi Maendeleo ya uhakika kwenye Jimbo la Musoma Vijijini.

## 2. UONGOZI NA MAWASILIANO JIMBONI

Uongozi bora daima unakuwa unayo mawasiliano mazuri ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya Maendeleo Endelevu kwa Jamii husika. Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameweka utaratibu mzuri wa kuwashirikisha Wananchi Vijijini kujitolea kuchangia Maendeleo yao kwa kushirikiana na Serikali yao kwa ngazi zote.

### 2.1 ZIARA ZA VIJIJINI ZA MBUNGE WA JIMBO

Ndani ya Miaka Mitatu na Nusu, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ametembelea Vijiji vyote 68 na Kata zote 21 zaidi ya mara tano na ziara zake zote ni za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni njia kuu ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020). Vilevile, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anatumia ziara hizi kupokea kero za Wananchi na kuzitatua na zingine kuzifikisha Serikalini.

## 2.2 WASAIDIZI WA MBUNGE WA JIMBO

Hawa wanazunguka ndani ya Vijiji vyote 68 na kila Msaidizi ana Vijiji vyake vya kazi, hivyo Wananchi hawana haja ya kumfuata Mbunge wa Jimbo badala yake Wasaidizi hawa ndio wanawafuata Wananchi huko huko Vijijini kusikiliza kero zao. Ili kurahisisha utendaji wa Wasaidizi hawa, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amewanunulia Vyombo na Vifaa vya kufanyia kazi kama vile (i) Pikipiki na Mafuta ya Pikipiki ya kila wiki, (ii) Kompyuta, (iii) Global Positioning System (GPS), (iv) Simu na Bando la muda wa maongezi.



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kulia) akiwatambulisha Wasaidizi wake kwa Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini*

## 2.3 MABARAZA YA WAZEE

Haya ni Mabaraza ya Ushauri, Ushawishi, Utamaduni na Maadili yaliyoundwa na Mbunge wa Jimbo ili kuboresha shughuli za Uhamasishaji wa Maendeleo katika Vijiji vyote 68 na Kata zote 21.

Mabaraza haya yanafanya kazi zake bila kuingilia Mihimili ya Serikali



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kushoto) akizungumza na Wazee wa Mabaraza ya Kata 21*

## 2.4 TOVUTI YA JIMBO

Ili kupanua Wigo wa Mawasiliano, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amefungua Tovuti ya Jimbo kwa ajili ya kuwajulisha Wananchi wa Jimboni, Nchini na Ulimwengu mzima kuhusu kazi za Maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini. Katika kitengo hiki yupo Mtendaji Mkuu wa Tovuti (Webmaster) ambaye ni Msaidizi mwingine wa Mbunge wa Jimbo. Tovuti hii ilizinduliwa rasmi tarehe 7 Mei 2016 katika Kijiji cha Saragana, Kata ya Nyambono na Anuani yake ni: www.musomavijijini.or.tz



*Wananchi wa Kijiji cha Saragana, Kata ya Nyambono wakishuhudia Tukio la Uzinduzi wa Tovuti ya Jimbo la Musoma Vijijini*

## 2.5 REDIO YA MTANDAONI (ONLINE RADIO)

Mawasiliano ya aina hii ya Redio ya Kisasa huwafikia Wananchi na kuwaeleza Miradi inayotekelezwa Jimboni na shughuli nyingine zote za Maendeleo. Jina lake ni Musoma Vijijini Online Voice News (MVOVN)




*Muonekano wa Musoma Vijijini Online Redio*

## 3 HUDUMA ZA JAMII

Huduma bora za Jamii ni nyenzo muhimu katika kuondoa umasikini na kuharakisha Maendeleo ya Wananchi. Katika kipindi cha Miaka Mitatu na Nusu (Januari 2016 - Juni 2019), Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, chini ya Uongozi wa Chama Cha Mapinduzi, ameendeleza jitihada zake za kuhakikisha kwamba Wananchi wanashirikiana kwa hali na mali na Serikali yao katika Uboreshaji wa Huduma za Kijamii Vijijini mwao.

### 3.1 SEKTA YA ELIMU

Jimbo la Musoma Vijijini lina Jumla ya Shule za Msingi 111 za Serikali (Government Primary Schools) na Shule 3 za Binafsi (Private Primary Schools). Pia Jimbo linazo Sekondari 18 za Serikali (Government Secondary Schools) na Shule 2 za Binafsi (Private Secondary Schools). Mbunge wa Jimbo, Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kushirikiana na Wananchi wote wamejiwekea MIPANGO ya kujenga na kuboresha Miundombinu ya Elimu kwenye Jimbo lao. Mipango hiyo inahusu:

#### 3.1.1 UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA

Kutokana na upungufu mkubwa wa Vyumba vya Madarasa unaopelekea mrundikano wa Wanafunzi Madarasani na wengine kusomea chini ya miti, Mbunge wa Jimbo anahamasisha Wananchi Vijijini kujitolea kujenga Vyumba Vipya vya Madarasa. Yeye mwenyewe anachangia fedha zake na vilevile Mfuko wa Jimbo (Fedha za Serikali) na Halmashauri ya Wilaya (Own Source) wanachangia ujenzi huu.



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (wa tatu kushoto) akishiriki kwenye Shughuli ya Ujenzi wa Vyumba 10 vya Madarasa na Ofisi 5 za Walimu katika S/M Kome B iliyoko Kijiji cha Kome, Kata ya Bwasi. Kushoto ni Diwani wa Kata ya Nyegina Mhe Majira Mchele akifuatiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mhe Charles Magoma. Hii ilikuwa tarehe 20/2/2017*

### 3.1.2 MICHANGO YA MBUNGE KWENYE UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA

Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ametoa MICHANGO YAKE BINAFSI kwenye Ujenzi wa Madarasa kwa kutumia njia mbili (2):

(i) Kugawa Saruji na Mabati moja kwa moja kwenye Shule za Msingi na Sekondari

(ii) Kwenda kwenye Shule za Msingi na Sekondari kupiga Harambee

Kwa upande wa Ugawaji wa Vifaa vya Ujenzi moja kwa moja mashuleni, Mbunge wa Jimbo amegawa Jumla ya Mifuko 5,884 ya Saruji kwa ajili ya Ujenzi wa zaidi ya Vyumba 196 vya Madarasa na Ofisi za Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari kwa Kata zote 21 na Vijiji vyote 68.

Michango ya Mbunge wa Jimbo kupitia HARAMBEE anazozipiga Vijijini imeainishwa kwenye Kiambatanisho Namba I kilichopo Ukurasa wa 89 – 110.



*Usambazaji wa Mifuko 5,884 ya Saruji iliyotolewa Jimboni na Mbunge wa Jimbo kwenye Shule za Msingi na Sekondari. Picha inaonesha Viongozi wa Kata ya Kabegi wakikabidhiwa Mifuko ya Saruji*

Shughuli ya Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa ilikwenda sambamba na Uezekaji wa Vyumba vya Madarasa. Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo aligawa Mabati yapatayo 3,220 ili kuezeka zaidi ya Maboma 59 ya Vyumba vya Madarasa na Ofisi za Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari.



*Shughuli ya Uezekaji wa Vyumba Vinne (4) vya Madarasa katika Shule ya Msingi Etaro baada ya kupokea jumla ya Mabati 144 kutoka kwenye Fedha za Mfuko wa Jimbo. Picha inaonesha Mafundi wakiwa katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa kazi hiyo.*

### 3.1.3 MICHANGO YA FEDHA ZA SERIKALI

Mbali ya michango ya Wananchi Vijijini, Mbunge wa Jimbo na Wadau wengine wa Maendeleo, Serikali inaendelea kutoa michango mikubwa ya Fedha kupitia Bajeti zake za kila Mwaka. Shule zote za Msingi za Serikali 111 na Sekondari zote 18 za Serikali zinapokea fedha na huduma nyingine za Serikali kila mwaka. Vilevile, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma yenye Jimbo la Musoma Vijijini na yenyewe inatoa fedha na huduma nyingine kwenye Shule zote za Serikali za Msingi na Sekondari zilizopo ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini. Orodha ya Matumizi ya Fedha za Serikali na zile za Halmashaauri yetu inapatikana kwenye Ofisi za Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.



*Majengo ya Shule ya Msingi Kurukerege yaliofadhiliwa kwa ushirika wa Fedha za Serikali, za Mbunge wa Jimbo, na NGUVUKAZI za Wananchi kwenye Kijiji cha Kurukerege, Kata ya Nyegina.*

### 3.1.4 MICHANGO YA MFUKO WA JIMBO

Fedha za Mfuko wa Jimbo ni fedha zinazotolewa na Serikali kwa matumizi ya miradi na shughuli za Maendeleo kwenye Majimbo yote ya Uchaguzi nchini. Mwenyekiti wa Mfuko huu ni Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi.

Katika Awamu ya Kwanza ya Fedha za Mfuko wa Jimbo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kushirikiana na Kamati ya Mfuko huo na Wananchi kwa pamoja walitenga kiasi cha Shilingi 27,500,000/= za Mfuko huo ili kukarabati Shule 2 za Msingi kama ifuatavyo:

- Ukarabati wa Vyumba 3 vya Madarasa ya Shule ya Msingi Nyetasho, Kijiji cha Nyambono, Kata ya Nyambono, Tsh 20,000,000/=

- Ukarabati wa Vyumba 2 vya Madarasa na Ofisi Shule ya Msingi Mabui Merafuru, Kijiji cha Mabui Merafuru, Kata ya Musanja, Tsh 7,500,000/=



*Majengo ya Vyumba vya Madarasa katika Shule Mpya ya Sekondari ya Kata ya Busambara inayojengwa kwa Michango ya Fedha za Wananchi (+ NGUVUKAZI), Mbunge wa Jimbo, Mfuko wa Jimbo, Halmashauri na TAMISEMI (Wizara)*

MICHANGO yote hiyo ILIYOAINISHWA hapo juu imewezesha Jimbo la Musoma Vijijini kujenga Vyumba VIPYA 450 vya Madarasa; Vyumba 350 vikiwa kwenye Shule za Msingi na 100 kwenye Shule za Sekondari. Haya ni MAFANIKIO makubwa ya kujivunia.

Orodha hapo chini inaonesha Shule za Sekondari Mpya zinazojengwa na zinazotarajiwa kujengwa:-

(i) Dan Mapigano Memorial Secondary School, Kata ya Bugoji
(ii) Busambara, Kata ya Busambara
(iii) Nyasaungu, Kata ya Ifulifu
(iv) Kigera, Kata ya Nyakatende
(v) Nyegina, Kata ya Nyegina
(vi) Ifulifu, Kata ya Ifulifu
(vii) Seka, Kata ya Nyamrandirira
(viii) Nyang’oma, Kata ya Mugango
(ix) Busamba, Kata ya Etaro



*Vyumba vya Madarasa ya Shule ya Sekondari ya Kata ya Bugoji (Dan Mapigano Memorial Secondary School) ambayo Mbunge wa Jimbo Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo aliweka Jiwe la Msingi tarehe 22 April, 2019. Michango ya ujenzi wake ni kama ile ya Sekondari ya Kata ya Busambara hapo juu*

### 3.1.5 UJENZI WA SHULE SHIKIZI

Kutokana na msongamano wa Wanafunzi kwenye Vyumba vya Madarasa ya Shule za Msingi, umbali mrefu wa Wanafunzi kutembea kwenda Vijiji vya jirani kupata Elimu ya Msingi, baadhi ya Vijiji vimeamua kujenga Shule zake za Msingi na wameanza kwa kujenga Shule Shikizi ambazo hapo baadae zitapanuliwa na kuwa Shule za Msingi kamili zenye Darasa la Awali hadi la Saba (Awali – VII).

Wananchi Vijijini kwa kushirikiana na Serikali na Mbunge wa Jimbo wanajenga Shule Shikizi ambazo hadi sasa zinafikia 10 na nyingine zimekamilika zipo tayari kupokea Wanafunzi. Shule hizo ni:

(i) Buraga Mwaloni, Kjiji cha Buraga, Kata ya Bukumi
(ii) Mwikoko, Kijiji cha Chitare, Kata ya Makojo
(iii) Gomora, Kijiji cha Musanja, Kata ya Musanja
(iv) Egenge, Kijiji cha Busamba, Kata ya Etaro
(v) Kihunda, Kijiji cha Kamguruki, Kata ya Nyakatende
(vi) Binyago, Kijiji cha Kabegi, Kata ya Ifulifu
(vii) Ziwa, Kijiji cha Mwiringo, Kata ya Busambara
(viii) Rwanga, Kijiji cha Kasoma, Kata ya Nyamrandirira
(ix) Karusenyi, Kijiji cha Mikuyu, Kata ya Nyamrandirira
(x) Kaguru, Kijiji cha Bugwema, Kata ya Bugwema
(xi) Buanga, Kijiji cha Buanga, Kata ya Rusoli

### 3.1.6 MICHANGO YA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (NGOs)

Serikali inashirikiana na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo yanapata fedha kutoka nchi za nje zinazoshirikiana na nchi yetu kwenye nyanja mbalimbali za Uchumi na Maendeleo. Mashirika hayo ni: PCI, EQUIP, EP4R na BMZ

#### 3.1.6.1 PROJECT CONCERN INTERNATIONAL (PCI)

Hili ni Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Jamii (PCI, Project Concern International). Shirika hili linajishughulisha na utoaji wa Mafunzo ya Kilimo kwa Wananchi walio katika Vikundi ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini ambao baadae huanzisha kilimo cha mazao ya chakula kama vile mahindi, viazi lishe, mpunga, mtama, mihogo na mazao ya biashara likiwemo zao jipya la Alizeti kwa kutumia mbegu walizopewa na Mbunge wao wa Jimbo. Shughuli nyingine zinazofanywa na PCI ni ujenzi wa Vyoo vya Wanafunzi, Matenki ya kuvuna maji ya Mvua na utoaji wa vitabu kwa Shule za Msingi Jimboni.

Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea kushirikiana na Shirika la PCI ambalo moja ya malengo yake makuu ni kutoa chakula mashuleni kupitia Vikundi vya Wakulima hali ambayo inaongeza hamasa kwa Wanafunzi kuhudhuria masomo na hatimae

kufanya utoro shuleni upungue sana na Wanafunzi kuwa na hamasa kubwa ya kupata Elimu.



*Kikundi cha Nguvukazi ambacho ni Miongoni mwa Vikundi vilivyoanzishwa na Shirika la PCI Kijijini Buanga kikiwa na mavuno ya mahindi kutoka shambani mwao*

### 3.1.6.2 EDUCATION QUALITY IMPROVEMENT PROGRAMME (EQUIP)

EQUIP (The Education Quality Improvement Programme) ni Mpango unaohusika na uboreshaji wa Miundombinu ya Elimu kwa kuchangia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa, Ofisi za Walimu, Matundu ya Vyoo vya Wanafunzi na Walimu pamoja na ujenzi wa Matenki ya kuvunia maji ya mvua kwa Shule za Msingi na Shule Shikizi zinazojengwa Musoma Vijijini. Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini, wanashirikiana na Serikali yao kupitia Mradi huu na Wafadhili wa EQUIP kufanikisha ujenzi wa Vyumba vya Madarasa. Vilevile, Wananchi wanajitolea kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji (NGUVUKAZI) ili kupunguza gharama za ujenzi kwenye Kijiji husika.

Wananchi na Viongozi ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini, kwa pamoja, wanaishukuru sana Serikali yetu kwa jitihada kubwa inazozifanya kwa kuwaunga mkono kwenye Miradi ya EQUIP na Miradi mingine ya Elimu Jimboni mwao.



*Jengo la Shule Shikizi Egenge, Kijiji cha Busamba, Kata ya Etaro lililojengwa na Mradi wa EQUIP kwa kushirikiana na Wananchi wa Kijiji hicho*

### 3.1.6.3 EDUCATION PROGRAMME FOR RESULTS (EP4R)

Education Programme For Results (EP4R) ni Mpango wa Kulipa Kulingana na Matokea unaolenga kuboresha kiwango cha Elimu kwa Shule za Sekondari nchini kote chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Jimbo la Musoma Vijijini kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Musoma pia limenufaika na Mpango huu kwa kujenga Vyumba vya Madarasa kwa Shule za Sekondari. Katika kuunga mkono jitihada za Serikali na kupunguza gharama za ujenzi,

Wananchi wanajitolea kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji (NGUVUKAZI).



*Jengo la Vyumba Vitatu vya Madarasa vilivyojengwa kwa Fedha za Mradi wa Lipa Kutokana na Matokeo (EP4R) katika Shule ya Sekondari Mkirira, Kata ya Nyegina*

### 3.1.6.4 BMZ

Mradi wa BMZ (The Federal Ministry of Economic Development and Cooperation) wa Ujerumani unahusika na ugawaji wa Vifaa vya Elimu kwa Wanafunzi wenye Ulemavu katika Kata 10 zilizo kwenye Mradi huu ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini. Kata hizo ni Bugwema, Bukima, Bukumi, Bwasi, Kiriba, Makojo, Murangi, Nyambono, Nyamurandirira na Suguti.

Vifaa vinavyotolewa na Mradi huu ni madaftari, kalamu, mabegi ya kubebea vifaa vya Shule, fimbo nyeupe kwa wenye ulemavu wa

macho, baiskeli za watu wenye ulemavu, miwani, miguu bandia na vifaa vingine wezeshi vikiwemo vifaa vya kusaidia usikivu mzuri. BMZ wanahusika pia na uundaji wa Vikundi vya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuwafadhili katika Miradi ya uzalishajii. Miongoni mwa Vikundi hivyo ni: ERUSULI SHIVYAWATA GROUP (Kata ya Kiriba), JIBIDISHE (Suguti), USHIRIKA (Bukumi), MTAZAMO (Murangi) na UPENDO (Bugwema)

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini anaendelea kushirikiana na BMZ kuhakikisha Mradi huu unaendelea kuwasaidia na kuwawezesha ki-uchumi watu wenye ulemavu na kuwaomba Wadau wengine waendelee kuwasaidia na kuwawezesha watu wenye ulemavu Jimboni.



*Makabidhiano ya Vifaa vya Elimu kutoka BMZ kwenye Kata ya Nyamrandirira*

### 3.1.7 UGAWAJI WA MADAWATI KWENYE SHULE ZA MSINGI

Kwa kipindi cha Miaka Mitatu na Nusu, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amegawa Madawati 8,000 aliyoyatengeneza kwa kutumia Kikosi cha SUMA - JKT Mwanza. Madawati hayo aliyagawa kwenye Shule za Msingi zote 111 za Jimbo la Musoma Vijijini. Kwa wakati huo, Mbunge wa Jimbo alitatua tatizo kubwa la uhaba wa madawati mashuleni.



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (wa pili kushoto) akipeana mkono na mmoja wa Wanafunzi katika Shule ya Msingi Rukuba iliyopo Kisiwani Rukuba ikiwa ni ishara ya Uzinduzi wa zoezi la Ugawaji wa Madawati 8,000 Jimboni humo*

## 3.1.8 UGAWAJI WA VITABU VYA SAYANSI NA KIINGEREZA

Ili kuwajengea Wanafunzi uwezo wa kujisomea, kuchambua mambo mbalimbali na kujiamini katika elimu waipatayo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo aligawa bure vitabu vya Sayansi na Kiingereza kutoka Marekani na Uingereza. Hadi sasa Jumla ya Kontena 5 zenye vitabu vyenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 2.5 vimeletwa na kugawiwa bure kwenye Shule zote za Msingi na Sekondari Jimboni. Vilevile, Shule za Binafsi za Sekondari na Msingi zimeomba na kugawiwa bure vitabu vya Mbunge wa Jimbo.

### 3.1.8.1 MGAO AWAMU YA KWANZA

Vitabu viligawiwa katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Mkirira tarehe 22/01/2016 ambapo Shule 10 za Msingi zilizofanya vibaya katika Mitihani ya kuhitimu Darasa la VII zilipewa upendeleo wa kugawiwa vitabu vingi zaidi. Aidha, kila Shule hiyo ilipata Box 10 na kila box ilikuwa na vitabu kati ya 20 na 30. Shule za Sekondari 20 zilipata Box 20 na kila box ilikuwa na vitabu kati ya 15 na 20.



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo (wa pili kushoto) akiwa katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Mkirira akikabidhi vitabu vya Sayansi na Kiingereza kwa Shule zote za Sekondari Jimboni na kwa Shule za Msingi 10 zilizopata matokeo mabaya ya Mitihani ya Darasa la Saba*

### 3.1.8.2 MGAO AWAMU YA PILI

Zoezi la ugawaji wa vitabu kwa Shule zote za Msingi na Sekondari awamu hii lilifanyika tarehe 07/05/2016 katika Viwanja vya Shule ya Msingi Kwibara, Kijijini Kwibara, Kata ya Mugango. Jumla ya Shule 111 za Msingi zilikabidhiwa Box 10 kwa kila Shule, wakati Shule 20 za Sekondari kila moja ilikabidhiwa Box 15.




*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kulia) akikabidhi Vitabu vya Sayansi na Kiingereza kwa Shule zote za Sekondari na Msingi za Jimboni katika Viwanja vya Shule ya Msingi Kwibara, Kata ya Mugango*

### 3.1.8.3 MGAO AWAMU YA TATU

Mgao wa awamu hii ulifanyika tarehe 20/09/2016 na ulihusisha Wabunge wote wa Mkoa wa Mara ambapo Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo aliwagawia vitabu Wabunge wote wa Mkoa wa Mara na wa kutoka Vyama vyote vya Siasa. Zoezi hilo lilifanyika katika Viwanja vya Shule ya Msingi Mkendo, Musoma Mjini. Jumla ya Vitabu 25,000 vya Masomo ya Sayansi na Kiingereza viligawiwa. Vilevile, Viongozi Wastaafu wanne (4) nao walipewa vitabu katika mgao huu.




*Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, Mhe John Heche (Chadema) kulia akitoa Shukrani kwa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo (CCM) wa pili kushoto mara baada ya kukabidhiwa Vitabu vya Shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya Shule za Jimbo lake la Tarime Vijijini.*

### 3.1.8.4 MGAO AWAMU YA NNE

Mgao huu ulihusisha Shule zilizo na Maktaba. Hii ikiwa ni mbinu ya kuhamasisha Shule zisizo na Maktaba zishawishike na zianze ujezi wa Maktaba zao. Mgao huu ulifanyika katika Viwanja vya Shule ya Msingi Etaro ambapo Jumla ya Shule 23 za Msingi zilikabidhiwa Box 230 na Shule 6 za Sekondari zilikabidhiwa Box 126.

Maktaba Mpya ya Kituo Cha Elimu cha Kanisa Katoliki Nyegina nayo ilipewa bure vitabu vya Mbunge wa Jimbo. Kituo hiki kinachojulikana kama, "Madaraka Nyerere Library and Community Resource Centre", kinashirikiana na Ofisi ya Mbunge kwa shughuli nyingi za maendeleo Jimboni.




*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kushoto) akiwa na Wanafunzi wa Shule ya Msingi Etaro huku akisoma Orodha ya Shule za Sekondari na Msingi zenye Maktaba zitakazokabidhiwa vitabu vya Sayansi na Kiingereza*



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kushoto) akizindua Jengo la Maktaba katika Shule ya Msingi Rukuba (Kisiwani). Maktaba hii ilijazwa Vitabu vya Sayansi na Kiingereza kwa ajili ya Wanafunzi, Walimu, Wanakijiji na Wageni watakaotembelea Kisiwa cha Rukuba*

## 3.2 SEKTA YA AFYA

Afya nzuri na imara ni muhimu sana kwa utendaji wa kazi uliokuwa na tija. Kwa hiyo, upatikanaji wa Huduma za Afya zilizo karibu na Wananchi wa Vijijini na zenye gharama nafuu ni muhimu kwa

utendaji kazi mzuri wenye kuimarisha Uchumi na Ustawi wa Jamii zetu. Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anaendelea kuwashawishi Wananchi waendelee kutekeleza Ilani ya CCM inayosema kila Kijiji kiwe na Zahanati moja na kila Kata moja iwe na Kituo cha Afya kimoja. Mbunge wa Jimbo, ameshirikiana na Serikali, Wananchi Vijijini, Madiwani, Wazaliwa wa Vijiji husika, baadhi ya Wafanyabiashara Vijijini na Wadau wengiine wa Maendeeo kwenye ujenzi na uboreshaji wa Miundombinu ya Afya Vijijini na kwenye baadhi ya Kata.

### 3.2.1 VITUO VYA AFYA

Jimbo la Musoma Vijijini lina Jumla ya Vituo viwili vya Afya vinavyotoa Huduma ambavyo ni: (i) Murangi na (ii) Mugango. Kituo kipya cha Afya cha Kata ya Nyambono kinaendelea kujengwa. Katika kuboresha na kuimarisha Miundombinu ya Vituo hivi, Mbunge wa Jimbo kwa kushirikiana na Serikali, Wananchi pamoja na Wadau wa Maendeleo amefanya mambo yafuatayo:

### 3.2.2 KITUO CHA AFYA MURANGI

Mbunge wa Jimbo amechangia Jumla ya Mifuko 400 ya Saruji, Mabati 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa Jengo la Mama na Mtoto. Katika Jitihada hizo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali ikiwemo Serikali ya Japan iliyochangia Jumla ya fedha za Kitanzania Shilingi Milioni 170, wamefanikiwa kupanua Kituo hiki. Fedha kutoka Serikali ya Japan zilitumika kujenga nyumba moja kubwa kwa ajili ya wafanyakazi

wawili (two in one), kichomea taka, shimo la kutupa kondo la nyuma na choo cha wagonjwa chenye matundu manne (4). Vile vile, Serikali ya Japan ilitoa Gari la Wagonjwa (Ambulance) ya kisasa. Ubalozi wa Australia nchini ulitoa vifaa tiba, magodoro na baiskeli za kubebea wagonjwa. Misaada yote hii inatokana na uelewano mzuri wa Mbunge wa Jimbo na Wafadhili wa ki-Mataifa.



*Sehemu ya Chumba cha kutolea Huduma ya Upasuaji katika Kituo cha Afya Murangi baada ya kufanyiwa maboresho makubwa na ya kisasa*



*Balozi wa Japan nchini Tanzania, Mhe Masaharu Yoshida (kulia) na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Ndugu Flora Rajabu Yongolo, wakisaini Hati za Makubaliano ya Msaada wa Shilingi Milioni 170 uliotolewa na Serikali ya Japan. Hii ilikuwa tarehe 10 March 2016, Kijijini Murangi*



*Matroni wa Kituo cha Afya cha Murangi, Ndugu Sabina Daudi akitoa Shukrani kwa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo (kushoto) baada ya kupokea Vifaa Tiba kwa ajili ya Kituo cha Afya Murangi*

### 3.2.3 KITUO CHA AFYA MUGANGO

Mbunge wa Jimbo Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amechangia Jumla ya Mifuko 400 ya Saruji kwa ajili ya ujenzi wa upanuaji wa Zahanati ya Mugango kuwa Kituo cha Afya. Serikali ilichangia Shilingi Milioni 400 kwa ajili ya ujenzi huu. NGUVUKAZI za Wananchi wa Kata ya Mugango zimetoa mchango mkubwa sana kuharakisha na kukamilisha ujenzi huu.



*Moja ya Majengo ya Kituo cha Afya cha Kata ya Mugango*

### 3.2.4 KITUO CHA AFYA NYAMBONO

Kituo hiki kinajengwa kwa michango ya Wazaliwa wa Kata ya Nyambono, Wananchi na Mbunge wa Jimbo. Mbunge wa Jimbo amechangia Mifuko 100 ya Saruji na Nondo 8 kwa ajili ya ukamilishaji wa Boma la Jengo la OPD. Michango zaidi bado inahitajika.



*Hatua ya Awali ya Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Nyambono*

### 3.2.5 ZAHANATI ZA SERIKALI

Jimbo la Musoma Vijijini kwa sasa lina jumla ya Zahanati 24 za Serikali na Zahanati 4 za Binafsi zinazotoa Huduma za Afya. Zahanati mpya 13 zinajengwa na Wanavijiji ndani ya Vijiji 13.

### 3.2.6 ZAHANATI ZINAZOTOA HUDUMA ZA AFYA

Zahanati 24 za Serikali zinatoa Huduma za Afya Vijijini ni:

1. Zahanati ya Bugoji, Kijiji cha Bugoji, Kata ya Bugoji
2. Bugunda, Kijijini Bugunda, Kata ya Bwasi
3. Bukima, Kijijini Bukima, Kata ya Bukima
4. Busungu, Kijijini Busungu, Kata ya Bulinga
5. Bwai, Kijijini Bwai Kwitururu, Kata ya Kiriba
6. Chitare, Kijijini Chitare, Kata ya Makojo
7. Etaro, Kijijini Etaro, Kata ya Etaro

8. Kiemba, Kijijini Kiemba, Kata ya Ifulifu
9. Kigera Etuma, Kijijini Kigera Etuma, Kata ya Nyakatende
10. Kiriba, Kijijini Kiriba, Kata ya Kiriba
11. Kome, Kijijini Kome, Kata ya Bwasi
12. Kurugee, Kijijini Buraga, Kata ya Bukumi
13. Kwikuba, Kijijini Kwikuba, Kata ya Busambara
14. Masinono, Kijijini Masinono, Kata ya Bugwema
15. Mwiringo, Kijijini Mwiringo, Kata ya Busambara
16. Nyakatende, Kijijini Kabegi, Kata ya Ifulifu
17. Nyambono, Kijijini Saragana, Kata ya Nyambono
18. Nyegina, Kijijini Nyegina, Kata ya Nyegina
19. Rukuba, Kisiwani Rukuba, Kata ya Etaro
20. Rusoli, Kijijini Rusoli, Kata ya Rusoli
21. Seka, Kijijini Seka, Kata ya Nyamrandirira
22. Suguti, Kijijini Kusenyi, Kata ya Suguti
23. Tegeruka, Kijijini Mayani, Kata ya Tegeruka
24. Wanyere, Kijijini Wanyere, Kata ya Suguti



*Zahanati ya Kijiji cha Kigera Etuma, Kata ya Nyakatende iliyojengwa kwa michango ya Wananchi, Wazaliwa wa Kijiji hicho, Mbunge wa Jimbo na Wadau wengine wa Maendeleo*

### 3.2.6.1 MICHANGO MINGINE YA MBUNGE WA JIMBO

Katika kuboresha Zahanati zilizotajwa hapo juu, Mbunge wa Jimbo amechangia MICHANGO mbalimbali ambayo ni pamoja na:

(i) Mifuko 50 ya Saruji kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya Mganga (two in one) katika Zahanati ya Kurugee

(ii) Mifuko 100 ya Saruji kwa ajili ya ujenzi wa Wadi ya Mama na Mtoto, Zahanati ya Bukima

(iii) Mifuko 50 ya Saruji kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati Mpya ya Kigera Etuma

(iv) Vifaa vya ujenzi (sink, nondo, wavu na mabomba) kwa ajili ya choo cha Zahanati ya Masinono

(v) Kugharamia samani (viti, meza na kulipa Shilingi 250,000/= kwa ajili ya Fundi wa kutengeneza samani) za Zahanati mpya ya Kijiji cha Mwiringo

(vi) Kukabidhi Darubini 1 katika Zahanati ya Kijiji cha Kigera Etuma
(vii) Kukabidhi Darubini 1 katika Zahanati ya Kisiwani Rukuba

Darubini 2 hizi zimeombwa na Mbunge wa Jimbo kutoka kwa Mdau wa Maendeleo na Mzaliwa wa Kijiji cha Rusoli, Daktari Bingwa Derick Nyasebwa wa Hospitali ya Uhuru ya Jijini Mwanza.



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kulia) akikabidhi Darubini*
*kwa Muuguzi wa Zahanati ya Kisiwa cha Rukuba, Ndugu Jovin Mafuru (kushoto)*

### 3.2.7 ZAHANATI BINAFSI

(i) Bwasi SDA, Kijijini Bwasi, Kata ya Bwasi
(ii) Mji Wa Huruma – Katoliki, Kijijini Kakisheri, Kata ya Nyakatende
(iii) Mugango KMT, Kijijini Nyang'oma, Kata ya Mugango
(iv) Rwanga KMT, Kijijini Kasoma, Kata ya Nyamrandirira

### 3.2.8 ZAHANATI MPYA ZINAZOJENGWA NA WANAVIJIJI

Baadhi ya Zahanati hizi (k.m Chirorwe, Maneke) tayari zimepokea michango ya fedha za Serikali.

(i) Burungu, Kijijini Bukumi, Kata ya Bukumi
(ii) Butata, Kijijini Butata, Kata ya Bukima
(iii) Bwai Kwitururu, Kijijini Bwai Kwitururu, Kata ya Kiriba
(iv) Chimati, Kijijini Chimati, Kata ya Makojo
(v) Chirorwe, Kijijini Chirorwe, Kata ya Suguti
(vi) Kakisheri, Kijijini Kakisheri, Kata ya Nyakatende
(vii) Kurukerege, Kijijini Kurukerege, Kata ya Nyegina
(viii) Kurwaki, Kijijini Kurwaki, Kata ya Mugango
(ix) Maneke, Kijijini Maneke, Kata ya Busambara
(x) Mkirira, Kijijini Mkirira, Kata ya Nyegina
(xi) Mmahare, Kijijini Mmahare, Kata ya Etaro
(xii) Nyasaungu, Kijijini Nyasaungu, Kata ya Ifulifu
(xiii) Nyegina, Kijijini Nyegina, Kata ya Nyegina

Ili kuharakisha ujenzi wa Zahanati mpya 13 zinazojengwa Jimboni, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo tayari amechangia MICHANGO mbalimbali ikiwa ni pamoja na Saruji kati ya Mifuko 50 na 350 kwa kila Zahanati zote zinazojengwa kasoro mbili (2) tu ambazo bado zipo hatua za awali za matayarisho. Mbunge wa Jimbo pia amechangia Nondo 40 katika Zahanati ya Nyasaungu.



*Wananchi wa Kijiji cha Kurwaki pamoja na Mbunge wa Jimbo, Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo wakiwa kwenye Harambee ya uezekaji wa Zahanati ya Kurwaki*



*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo akizungumza na Wananchi wa Kijiji cha Nyasaungu baada ya Harambee ya Ujenzi wa Zahanati yao*

### 3.2.9 UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA

Wananchi na Viongozi wa ngazi mbalimbali akiwemo Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, wanaishukuru sana Serikali yao chini ya

Uongozi wa Rais Dkt John Joseph Pombe Magufuli kwa kutoa Shilingi bilioni **1.5** kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya inayojengwa kwenye Kitongoji cha Kwikonero, katika Kijiji cha Suguti, Kata ya Suguti. Wananchi kupitia Viongozi wa Kata na Vijiji wamekubaliana kuchangia Shilingi Milioni 2 kila Kijiji na Mbunge wa Jimbo yuko tayari kuchangia ujenzi huu muda ukiwadia.



*Moja ya Majengo ya Hospital ya Wilaya inayojengwa katika Kitongoji cha Kwikonero, Kijijini Suguti, Kata ya Suguti*

### 3.2.10 MATIBABU KUTOKA KWA MADAKTARI BINGWA WA CHINA

Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ametumia uhusiano wake mzuri na Wataalamu wa China na Serikali yao kuwaomba Madaktari Bingwa wa China kutoa bure huduma za matibabu kwa Wanavijiji Jimboni. Huduma hizo zimetolewa mara tano kama ifuatavyo:

- ❖ Kituo cha Afya Murangi, Marchi 6-7, 2016,
- ❖ Zahanati ya Mugango, Juni 25-26, 2016,
- ❖ Zahanati ya Nyakatende, Julai 22-23, 2016,

- Zahanati ya Nyambono, Mei 7-8, 2017,
- Zahanati ya Kwikuba, Mei 9-10, 2017.



*Prof Muhongo akiwatambulisha Madaktari Bingwa kutoka nchini China waliowasili Jimboni kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu katika Zahanati ya Mugango. Hii ilikuwa tarehe 25-26/06/2016*



*Daktari Bingwa kutoka nchini China akimchunguza mtoto mgonjwa kwenye Zahanati ya Kijiji cha Kwikuba*

### 3.2.11 MAGARI YA KUBEBEA WAGONJWA (AMBULANCES)

Kwa kipindi cha Miaka Mitatu na Nusu, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameleta jumla ya Magari Matano (5) ya Wagonjwa na kuyagawa katika Kituo cha Afya Murangi na kwenye Zahanati za Vijiji vya Masinono (Kata ya Bugwema), Kurugee (Kata ya Bukumi), Mugango (Kata ya Mugango) na Nyakatende (Kata ya Ifulifu)



*Gari la kisasa la Wagonjwa la Kituo cha Afya Murangi ambalo lilikabidhiwa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, tarehe 10 Machi, 2016*




*Gari la Wagonjwa lililokabidhiwa na Mbunge wa Jimbo Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo katika Zahanati ya Mugango ambayo imepanuliwa na kuwa Kituo cha Afya*



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kulia) akikabidhi Nyaraka za Gari la Wagonjwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma, Ndugu Flora Yongolo katika Zahanati ya Nyakatende iliyopo Kata ya Ifulifu*



*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kushoto) akikabidhi Gari la Wagonjwa katika Zahanati ya Masinono, Kata ya Bugwema. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney akifuatiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Ndugu Flora Yongolo*




*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (wa kwanza kulia) akifuatiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma, Ndugu Flora Yongolo na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dkt. Vicent Naano Anney (wa pili kushoto) wakiwakabidhi Gari la Wagonjwa la Zahanati ya Kurugee, Kata ya Bukumi*

## 3.2.12 MICHANGO YA MASHIRIKA YA UMMA

Moja ya Mashirika ambayo yamekuwa yakitoa michango yao mikubwa katika kuinua Maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini ni National Microfinance Bank (NMB). Benki hii imekuwa ikitoa vifaa tiba katika Zahanati za Jimbo la Musoma Vijijini; kwa mfano, NMB imechangia vitanda vitano na magodoro katika Kituo cha Afya Mugango.



*Benki ya NMB ikitoa vifaa tiba na vitanda vitano kwenye Kituo cha Afya Mugango. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, Ndugu Frola Rajab Yongoro, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney, Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Musoma, Ndugu Sebastian Kayaga pamoja na Meneja wa Miradi na Uwajibikaji kwa Jamii wa Benki ya NMB, Bi Lilian Kisamba*

# 4 HUDUMA ZA KIUCHUMI

## 4.1 SEKTA YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI

Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kushirikiana na Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ameendelea kuishirikisha Jamii katika kushiriki shughuli za uzalishaji hususani kupitia Kilimo, Uvuvi na Ufugaji ili kuimarisha

kipato cha kaya na cha mtu mmoja mmoja, kutoa AJIRA kwa Wanavijiji wakiwemo Vijana.

## 4.1.1 KILIMO

Jimbo la Musoma Vijijini lina takribani Kaya 52,830, kati ya hizo Kaya zinazotegemea kilimo ni 42,264 ambayo ni sawa na Asilimia 80 ya Kaya zote. Kaya nyingine 10,566 ambayo ni sawa na Asilimia 20 zinajihusisha na shughuli nyingine za kiuchumi. Kwa hiyo, Sekta ya Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi kwa wakazi wa Musoma Vijijini ambao wanajishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali yakiwemo:

(i) Mazao ya chakula: mihogo, mtama, mahindi, mpunga, viazi vitamu, matunda na mbogamboga

(ii) Mazao ya biashara: pamba, alizeti, mpunga, mahindi, mihogo, matunda na mbogamboga

## 4.1.2 KILIMO CHA UMWAGILIAJI

Sehemu ya Fedha za Mfuko wa Jimbo ya Mwaka 2015/2016, ilitumika kununua Vifaa vya Kilimo cha Umwagiliaji ambavyo viligawiwa bure kwenye VIKUNDI 15 vya Wakulima, wengi wao wakiwa Vijana. Pampu 15, mipira yake, na mbegu viligawiwa.




*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kulia) akikabidhi Pampu 15, mipira yake na mbegu kwa Vikundi 15 vya Wakulima wa Kilimo cha Umwagiliaji.*



*Kikundi cha No Sweat No Sweet kilichopo Kijijini Bugunda, Kata ya Bwasi baada ya kuvuna matikiti maji shambani mwao. Hiki ni moja kati Vikundi 15 vilivyopokea Pampu zilizonunuliwa kwa Fedha za Mfuko wa Jimbo*

## 4.1.3 MRADI WA BONDE LA BUGWEMA

Mradi mkubwa wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Bonde la Bugwema, ulionzishwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu J. K. Nyerere,

unafufuliwa. Kilimo cha umwagiliaji kwenye Bonde la Bugwema lenye ukubwa wa Ekari 5,075 utakuwa wa ushirika kati ya Wanavijiji, Halmashauri na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania itajenga miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya Wananchi kufanya kilimo cha umwagiliaji ndani ya Bonde la Bugwema. Mazao yatakayozalishwa kwenye Bonde hili ni: mpunga, mahindi, vitunguu, dengu, alizeti na pamba. Aidha TADB itatoa vifaa vya Kilimo kwa Wakulima kwa Makubaliano ya Mkataba baina ya pande zote. Utaratibu wa kurejesha Mikopo utahakikisha unawanufaisha Wakulima watakaokuwa ndani ya Mradi huu. Pembejeo zitakazotolewa na TADB ni zana za kisasa za kilimo, mbegu na mbolea. Masoko na huduma nyingine pale zitakapokuwa zinahitajika, navyo vitatolewa na TADB.

### 4.1.4 KILIMO CHA ALIZETI

Licha ya zao la PAMBA kuwa zao la kibiashara kwa miaka mingi ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini, uzalishaji wake umeshuka. Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, amewashawishi Wakulima Jimboni kuanza kulima zao jipya la ALIZETI badala ya kutegemea zao la aina moja tu la Pamba.

ALIZETI ni zao ambalo linastawi vizuri kwenye maeneo mengi Jimboni. Mbunge wa Jimbo, Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, kwa misimu mitatu mfululizo amegawa bure mbegu za ALIZETI kwenye Kata zote 21 kama ifuatavyo:.

- Msimu wa 2016/2017: Kg 4,682 (Tani 4.68)
- Msimu wa 2017/2018: Kg 4,974 (Tani 4.97)
- Msimu wa 2018/2019: Kg 1,243 (Tani 1.24)

Jumla ya Mchango wa Mbunge wa Jimbo = Kg 9,656 sawa na Tani 9.66



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (wa pili kulia) akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney (kushoto) wakati wa uzinduzi wa ugawaji wa Mbegu za ALIZETI Jimboni*

Mbunge wa Jimbo, anatoa shukrani nyingi kwa Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ambayo ilitoa Jumla ya Tani 10 za mbegu za ALIZETI kwa Msimu wa 2018/2019



*Viongozi mbalimbali wa Serikali wakikagua Shamba la ALIZETI katika Shule ya Msingi Busekela iliyopo katika Kijiji cha Busekela, Kata ya Bukumi*

### 4.1.4.1 MITAMBO YA KUKAMUA MBEGU ZA ALIZETI

Ili kuboresha kilimo cha ALIZETI na kukifanya kuwa na mvuto kwa Wakulima, Kampuni 2 za Watu Binafsi zimefunga Mitambo ya kukamua mbegu za ALIZETI ili kuongeza thamani kwenye mnyororo mzima wa kilimo cha ALIZETI kwenye Jimbo la Musoma Vijijini. Mitambo hiyo imejengwa kwenye Vijiji vya Kusenyi na Saragana. Aidha, Soko la ALIZETI linapatikana kwa uhakika ndani ya Mkoa wa Mara zikiwemo Wilaya za Musoma, Butiama na Bunda.



*Mtambo wa kukamua mbegu za ALIZETI katika Kijiji cha Kusenyi, Kata ya Suguti ukiwa tayari kwa ajili ya kuzalisha Mafuta ya ALIZETI inayolimwa na Wananchi wa Musoma Vijijini.*

## 4.1.5 KILIMO CHA MIHOGO

Mbali ya zao la mihogo kuwa la chakula kikuu Jimboni, Wakulima wameitikia wito wa kupanua na kuboresha uzalishaji wa mihogo kwa matumizi ya chakula na biashara. Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amenunua na kugawa bure Magunia 796 ya mbegu ya mihogo aina ya Mkombozi. Kila gunia lilikuwa na pingili 1,000 na zimegawiwa bure mara mbili:

- Mwaka 2016/2017: Gunia 446
- Mwaka 2017/2018: Gunia 350



*Wananchi wa Kata ya Nyegina wakikabidhiwa mbegu za mihogo kwa ajili ya kulima na kuzalisha mbegu zaidi kwa matumizi ya eneo hilo.*



*Mkulima Mashuhuri wa zao la mihogo akipalilia shamba la mihogo lililotumia mbegu aina ya Mkombozi. Hapa ni Kijijini Murangi, Kata ya Murangi.*

## 4.1.6 KILIMO CHA MTAMA

Katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula Jimboni, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, ameendelea kuhamasisha Wananchi kushiriki katika uboreshaji wa kilimo cha mtama ili

kukabiliana na majira ya mvua zisizotabirika. Mbunge wa Jimbo alipokea maombi ya Wananchi ya kusaidiwa mbegu za mtama. Mbunge wa Jimbo alilipokea ombi hilo na kulitekeleza kikamilifu, kwa kugawa bure mbegu za mtama kwa Wakulima Vijijini kwa misimu miwili kama ifuatavyo:

- Februari 2017: Kg 900 (Tani 0.9)
- Agosti 2018: Kg 6,800 (Tani 6.8)



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (aliyevaa flana nyeupe - katikati) akipeana mkono na mmoja wa Wakulima baada ya kukabidhi mbegu za mtama kwa Wananchi katika Kijiji cha Nyabaengere, Kata ya Musanja*

## 4.1.7 UBORESHAJI WA ZANA ZA KILIMO

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kupitia vikao mbalimbali vya Wananchi na Wataalamu wa kilimo wamepanga kupunguza utumiaji wa jembe la mkono.

Taratibu hizo ziinafanyika chini ya usimamizi wa Wataalamu wa Kilimo ngazi za Vijiji, Kata na Halmashauri kama ifuatavyo:

- ❖ TREKTA - Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS), Vikundi vya Wakulima na Wakulima binafsi wanashawishiwa waombe Mikopo ya Matrekta. Ofisi ya Kilimo ya Halmashauri inatoa ushauri kwa Wakopaji wa Matrekta.
- ❖ PLAU - Wakulima Vijijini wanashawishiwa waunde Vikundi vya kilimo vikiwajumuisha Wanavijiji wenye ng'ombe ili majembe (PLAU) ya kukokotwa na ng'ombe yatafutwe na kutolewa kwa mkopo. Mbunge wa Jimbo ndiye anayesimamia zoezi la upatikanaji wa PLAU zitakazohitajika.

## 4.2 UVUVI

Mbunge wa Jimbo, kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Musoma wameendelea kuwashirikisha Wananchi kwenye Uvuvi Bora unaozingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali.

Mbunge wa Jimbo ameshiriki vikao kadhaa vilivyohusisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi vilivyokuwa vikihusisha Wavuvi wanaotoka maeneo ya Ziwa Viktoria ili kujadili masuala mbalimbali yahusuyo Sekta ya Uvuvi. Pia, Mbunge wa Jimbo amefikisha Serikalini

maombi ya Boti ya Doria ambayo ikipatikana itaboresha usalama wa Wavuvi wa Jimbo la Musoma Vjijini.

## 4.3 UFUGAJI

Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Musoma imeboresha Sekta ya Ufugaji kwa kutoa Elimu kwa Wafugaji wa Jimbo la Musoma Vijijini kuhusu Ufugaji wa kuku wa nyama na mayai. Katika Halmashauri ya Musoma, Serikali imetoa madawa kwa ajili ya majosho manane (8) na kugawanywa katika majosho manne (4) ya Saragana, Bugwema, Mugango na Bugoji. Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo tayari amefikisha maombi mengine Serikalini ya kuongeza majosho na upatikanaji wa madawa ili kukidhi mahitaji ya Wafugaji na mifugo yao. Pia, Wananchi wamehamasishwa kuchanja mbwa na paka ili kuepuka magonjwa ya mapele ya ngozi, homa ya mapafu na kimeta.

# 5. MIRADI YA MAJI, UMEME NA BARABARA

Mbunge wa Jimbo ameendelea kuiomba Serikali kutekeleza Miradi ya Maji, Umeme na Barabara ndani ya Jimbo lao. Serikali imezidi kupiga hatua kubwa kufikisha huduma hizi kwa Wananchi huko Vijijini.

## 5.1 MIRADI YA MAJI

### 5.1.1 MIRADI YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

#### (i) MRADI WA BULINGA - BUSUNGU

Mradi huu wenye Vijiji vitano (5) vya Bulinga, Bujaga, Busungu, Bukima na Kwikerege umegawanywa kwenye makundi mawili (2 Lots) ili kuharakisha utekelezaji wake kama ifuatavyo:

**Kundi I (Lot I)**

**Bulinga - Bujaga**: Maji yatachukuliwa kutoka Kijiji cha Bujaga kwa ajili ya kusambaza kwenye Vijiji vya Bujaga na Bulinga, vyote vya Kata ya Bulinga. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi MEDES COMPANY Ltd na gharama yake ni Tsh. 1,812,675,036 (Tsh 1.81 bilioni). Mradi huu ulizinduliwa kwenye Mbio za Mwenge za mwaka huu (2019)



*Mabomba yanayoandaliwa kwa ajili ya usambazaji wa maji wa Mradi wa Bulinga - Busungu unaotekelezwa katika Kata ya Bulinga*

**Kundi II (Lot II)**

**Busungu – Bukima - Kwikerege**: Maji yatachukuliwa kutoka Kijiji cha Bujaga na kusambazwa Vijijini Busungu (Kata ya Bulinga), Bukima (Kata ya Bukima) na Kwikerege (Kata ya Rusoli). Utekelezaji wa Mradi wa usambazaji wa maji kwenye Vijiji hivi vitatu (3) unaendelea kwa kasi ya kuridhisha. Mradi wa Busungu – Bukima - Kwikerege: unagharimu Shilingi 1, 022, 531, 876 (Tsh

1.02 bilioni), unatekelezwa na Mkandarasi EDM NETWORK LTD JV FAU CONSTRUCTION LTD.



*Moja ya Vituo 18 vya kuchotea Maji vikiendelea kujengwa katika Mradi wa Maji wa Bulinga - Busungu unaotekelezwa katika Kata ya Bulinga*

**(ii) MRADI WA WANYERE**

Mradi huu utahudumia Vijiji vinne vya Kata ya Suguti ambavyo ni Suguti, Kusenyi, Wanyere na Chirorwe. Utekelezaji wa Mradi huu unaendelea.

**(iii) MRADI WA MAKOJO – CHITARE**

Vijiji vitakavyohudumiwa na Mradi huu ni: Makojo na Chitare.

**(iv) UPANUZI WA MRADI WA BUKUMI - BURAGA KUELEKEA BUSEKELA**

Baada ya kukamilika kwa Mradi wa Maji wa Bukumi – Buraga ambao awali ulikuwa unahudumia Vijiji vya Bukumi na Buraga, Mradi huu sasa unapanuliwa kuelekea Kijiji cha Busekela. Hivyo,

baada ya upanuzi huu kukamilika, Mradi utakuwa unahudumia Vijiji vitatu ambavyo ni: Bukumi, Buraga na Busekela, vyote vya Kata ya Bukumi.

**(v) MRADI WA BADEA (MUGANGO – KIABAKARI – BUTIAMA)**

Mradi huu wa Bomba la Maji safi na salama la kutoka Ziwa Viktoria (Mugango, Musoma Vijijini) hadi Wilaya ya Butiama (Kiabakari – Butiama) utaanza kutekelezwa mwaka huu (2019). Vijiji vya Kata za Mugango na Tegeruka vitakuwa vya kwanza kusambaziwa maji kutoka kwenye Bomba hili. Huu ni Mradi mkubwa na muhimu wenye thamani ya Shilingi bilioni sabini (Tsh 70 bilioni au US$ 30.69 million).

**(vi) MRADI WA MUWASA**

Maji yanayozalishwa na MUWASA kutoka Ziwa Viktoria kwa ajili ya Mji wa Musoma ni mengi mno na matumizi yake kwa sasa ni takribani 50% ya maji yanayozalishwa. Kwa hiyo, Serikali imeamua Vijiji vya Jimbo la Musoma Vijijini na Jimbo la Butiama visambaziwe maji hayo ya ziada. Kwa upande wa Jimbo la Musoma Vijijini, Vijiji vyote vya Kata za Etaro, Nyegina, Nyakatende na Ifulifu vitasambaziwa maji hayo na tayari Mradi unatekelezwa.

**(vii) MRADI WA MAZIWA MAKUU**

Vijiji thelathini na tatu (33) vya Jimbo la Musoma Vijijini vilivyoko karibu na Ziwa Viktoria, vimo kwenye Mradi huu. Usanifu umekamilika na Serikali inajipanga ianze utekelezaji wake.

### 5.1.2 MIRADI YA MAJI AMBAYO USANIFU UMEKAMILIKA

#### (i) MRADI WA MIKUYU

Katika utekelezaji wa Mradi huu, maji yatachukuliwa Kijijini Chumwi na kusambazwa kwenye Vijiji vinane (8) ambavyo ni Chumwi, Mikuyu, Mabui Merafuru, Nyambono, Saragana, Kanderema, Bugoji na Kaburabura.

#### (ii) MRADI WA BUGWEMA

Vijiji vitakavyohudumiwa na Mradi huu ni Bugwema, Masinono, Muhoji na Kinyang'erere, vyote vya Kata ya Bugwema.

Miradi hii miwili ambayo usanifu wake umekamilika (Mradi wa Mikuyu na Mradi wa Bugwema), imewasilishwa Serikalini na Mbunge wa Jimbo anafuatilia upatikanaji wa fedha za utekelezaji wake.

Vilevile, Mbunge wa Jimbo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, amewasilisha Serikalini Ombi la Mradi wa Visima 20.

### 5.2 MRADI WA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI (REA)

Serikali kupitia Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA) imepiga hatua kubwa ya usambazaji wa umeme katika Vijiji vya Jimbo la Musoma Vijijini ambapo hadi kufikia Juni 2019, Jumla ya Vijiji 63 kati ya Vijiji 68 tayari vimeshapata umeme. Pia jumla ya Vitongoji 149 kati ya Vitongoji 374 vimeshapatiwa umeme

Hata hivyo, katika hatua ya utekelezaji wa Mradi wa REA III Awamu I, kwa upande wa Musoma Vijijini, Jumla ya Vijiji vinavyotakiwa kusambaziwa umeme ni 30, ambavyo tayari vimewashwa ni 7. Aidha Vijiji vinavyotarajiwa kuunganishiwa

umeme kwa mwezi wa Julai 2019 ni vinne (4). Vijiji hivyo ni Kakisheri, Nyang'oma, Kurukerege na Kigera Etuma. Waziri wa Nishati, Mhe Dkt Medard Kalemani alirudia kusisitiza ahadi ya Serikali isemayo Vijiji vyote 68, na Vitongoji vyake vyote 374 vitapatiwa umeme ifikapo mwakani (2020).



*Waziri wa Nishati, Mhe Dkt Medard Kalemani akiwasha umeme Kijijini Nyakatende, Kata ya Nyakatende wakati alipokuwa akikagua utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa REA III ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini*

## 5.3 MIRADI YA BARABARA

### 5.3.1 UJENZI WA BARABARA YA LAMI (TANROADS)

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa jitihada zake za kushirikiana na Serikali ya Awamu ya Tano, amekuwa akifuatilia kwa ukaribu sana Mradi huu wa Barabara ya Lami ya Musoma – Mugango – Makojo - Busekela. Hivyo, Jimbo la Musoma Vijijini limepiga hatua kubwa sana hasa ile ya kupata, "No Objection" kutoka Wizarani - yaani Wizara imeridhia Mradi huo utekelezwe. Mbunge wa Jimbo anafuatilia kila hatua ya matayarisho na anawasiliana na ngazi zote za Serikali. Ahadi ya Rais wetu, Mhe Dkt John Pombe Joseph Magufuli ya kujenga barabara hili la Kilomita 92 kwa kiwango cha lami imeanza kutekelezwa.

### 5.3.2 MATENGENEZO YA BARABARA (TANROADS)

Jimbo la Musoma Vijijini lina barabara mbili zinazohudumiwa na TANROADS ambazo ni Musoma - Mugango - Makojo - Busekela. Fedha za matengenezo ya kawaida zimeendelea kuwepo kwenye Bajeti za Serikali za kila Mwaka.

Barabara ya pili ni ile ya Murangi – Bugwema – Manyamanyama (Bunda) ambayo imeendelea kuhudumiwa na TANROADS kwa matengenezo ya mara kwa mara. Barabara hii inapitika mwaka mzima.

Mbunge wa Jimbo anashirikiana na TANROADS kwa karibu sana kuhakikisha kwamba barabara kuu hizi za Jimbo zinapata Bajeti Serikalini kwa matengenezo yake.

### 5.3.3 BARABARA VIJIJINI (TARURA)

Barabara zote za Vijijini kwa sasa zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) na wanajitahidi kuhakikisha barabara hizi zinatengenezwa na zinapitika kwa urahisi kwa mwaka mzima. Matengenezo hayo ni pamoja na ujenzi wa madaraja yaliyoharibika. Mbunge wa Jimbo anawasiliana na TARURA kwa karibu sana ikiwemo ufuatiliaji wa Bajeti yao (TARURA) ndani ya Serikali.



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe Injinia Edwin Ngonyani (aliyesimama) akizungumza na Wananchi wa Kijiji cha Bukima (hawapo pichani) kuhusu ujenzi wa barabara ya lami ya Musoma – Mugango – Makojo - Busekela*

## 6. USAFIRI JIMBONI (MAGARI YA MBUNGE)

Ili kurahisisha zoezi la usafirishaji wa vifaa mbalimbali vya ujenzi na shughuli nyingine za Jimbo, Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo alinunua MAGARI mawili (2) na kuyakabidhi Jimboni kwa ajili ya shughuli za Maendeleo ya Jimbo kama ifuatavyo:

**(i) KENTA 1**: Kwa ajili ya usombaji wa vifaa mbalimbali vya ujenzi na kutoa usafiri kwa wenye mahitaji ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

**(ii) TIPA 1**: Kufanya shughuli za ujenzi ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

Halmashauri nayo wanatumia MAGARI haya kwa uhamisho wa wafanya kazi wake na kwa shughuli zake za ujenzi na nyinginezo.



*Gari (KENTA) iliyotolewa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa ajili ya shughuli za Jimbo.*



*Gari (TIPA) iliyotolewa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa ajili ya shughuli za Jimbo.*

**7. UTUNZAJI WA MAZINGIRA**

Katika zoezi zima la kupambana na mabadiliko ya tabianchi, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma Dr Vincent Naano Anney, Mbunge wa Jimbo la Musoma Mjini, Mhe Vedastus Mathayo na Kikundi cha Wana Nyanja Development Initiative (NDI), wameanzisha Mradi wa uoteshaji wa miche ya miti kwa ajili ya kupandwa katika Vijiji vyote vya Jimbo la Musoma Vijijini na Mitaa ya Musoma Mjini. Mradi huu unakusudia kuotesha MICHE ya miti zaidi ya Milioni kumi (10).



*Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dr Vincent Naano Anney akishiriki katika zoezi la upandaji miti katika Shule ya Msingi Bwai Kumusoma ikiwa ni ishara ya Uhamasishaji wa Wananchi kushiriki upandaji wa miti katika maeneo mbalimbali ya makazi, mashamba na maeneo ya Taasisi za Serikali na za Binafsi*

## 8. MICHEZO NA UTAMADUNI

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ameendelea kushirikiana na Wananchi wa Wilaya ya Musoma kwenye masuala ya Michezo na Utamaduni.

### 8.1 KUDUMISHA NA KUKUZA UTAMADUNI

Kwenye mipango ya kudumisha na kukuza utamaduni wetu, Mbunge wa Jimbo, ameunda Mabaraza ya Wazee katika ngazi ya Kata na Vijiji.

Mabaraza haya yanajulikana kama, “Baraza la Wazee la Ushauri, Ushawishi, Utamaduni na Maadili”. Kazi yake ni kushauri na kushawishi utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwenye Vijiji na Kata zao. Vilevile, yanatoa ushauri kwenye udumishaji wa utamaduni wetu wa asili.

Vilevile, Mbunge wa Jimbo ameanzisha mashindano ya KWAYA na NGOMA za ASILI ya kila mwaka kusheherekea Sikukuu ya Wakulima ya NANENANE.

Mashindano ya KUPIGA KASIA nayo yapo na yalianzishwa na Mbunge wa Jimbo. Washindi wa mashindano yote haya wanapewa zawadi na mtayarishaji wake ambaye ni Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo.



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (wa tatu kushoto) akiwa na Viongozi mbalimbali wa Wilaya wakishuhudia Mashindano ya Kwaya na Ngoma za Asili yaliyofanyika katika Kijiji cha Suguti, tarehe 8/8/2016.*



*Kikundi cha KIWAJAKI kutoka Kata ya Kiriba kikishiriki katika Mashindano ya Sherehe za Nanenane Kijijini Suguti. Ilikuwa tarehe 8/8/2016*



*Kikundi cha Kwaya kutoka Kata ya Bugoji kilishika nafasi ya kwanza katika Mashindano ya Nanenane yaliyofanyika Agost 8, 2016 katika Kijiji cha Suguti, Kata ya Suguti*




*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma,Mhe Charles Magoma (kushoto) ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Mugango akikabidhi zawadi kwa Washindi wa kwanza katika Mashindano ya Kupiga Kasia tarehe 31/12/2016*

## 8.2 MPIRA WA MIGUU

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ni Mshiriki mzuri katika masuala ya mchezo wa Mpira wa Miguu ambapo amekuwa akitoa michango mbalimbali ili kuhakikisha timu zetu zinacheza katika mazingira ya kuridhisha na kupata ushindi.

Katika eneo hili, Mbunge wa Jimbo amekuwa ni mmoja ya Wafadhili Wakuu wa Timu ya Biashara United Mara. Baadhi ya michango aliyotoa kwa Timu hii ni:

- ❖ Kulipia kodi ya pango na kununua magodoro, mito na mashuka kwa wachezaji.

- ❖ Kutoa motisha kwa wachezaji na viongozi wote
- ❖ Kununua chakula cha wachezaji na viongozi wao
- ❖ Kuchangia usafiri wa wachezaji na viongozi wa Timu

Kwa upande mwingine, Mbunge wa Jimbo amewahi kutoa mipira na jezi kwa timu zote za Vijana katika Vijiji vyote 68 na mashuleni.
Mbali na Timu hiyo ya Biashara, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini anatarajia kuunda Timu ya Jimbo la Musoma Vijijini kupitia Mashindano ya vijana Vijijini, Katani hadi Jimbo kwa kuchagua vipaji na hatimaye kuwa na hazina kubwa ya vijana watakaoweza kuchukuliwa na Timu ya Biashara United na timu nyingine kubwa za ndani na nje ya nchi.




*Wachezaji wa Timu ya Mpira wa Miguu ya Biashara United Mara ambayo inashiriki Ligi kuu ya Tanzania Bara (TPL), 2018/2019*

## 9. USHIRIKI KWENYE MASUALA YA KIJAMII

Mbunge wa Jimbo amekuwa mstari wa mbele katika kuguswa na kushirikiana na Jamii yake hasa katika matatizo mbalimbali kama ya maafa na misiba. Yafuatayo ni baadhi ya MATUKIO ambayo Mbunge wa Jimbo ameweza kuwafikia na kuwasaidia Wananchi Vijijini mwao:

(i) Kutembelea na kuzipa pole familia 5 za Kijiji cha Kiemba zilizokumbwa na adha ya kubomokewa na nyumba na nyingine kuezuliwa mapaa. Mbunge wa Jimbo alichangia mabati, saruji na misumari kwa ajili ya kujenga nyumba zilizobomoka.

(ii) Kuwapa pole waathirika wa kimbunga katika Kijiji cha Bukima, Kata ya Bukima na kutoa msaada wa mabati, mbao, saruji na misumari kwa familia moja ya mama mzee (mjane).

(iii) Kuwatembelea waathirika wa mafuriko na kimbunga katika Vijiji vya Busekela, Bukumi, Rusoli, Buanga na Kastam ambapo alitoa msaada wa chakula kwa familia 11 za Kijiji cha Bukumi.

(iv) Kuwapa pole waathirika wa mvua iliyoambatana na upepo mkali katika Kata ya Ifulifu. Alitoa msaada wa chakula kwa kaya zipatazo 45 ambazo nyumba zao ziliezuliwa na mazao kuharibika mashambani.

(v) Kutoa msaada wa taa na chaja za simu zinazotumia Mionzi ya Jua kwa familia tatu zilizopata matatizo ya kimbunga Kijijini Kiemba.

(vi) Kuwapa pole waathirika wa kimbunga Kijijini Kurukerege, Kata ya Nyegina na kutoa msaada kwa Mama Mjamzito aliyeangukiwa na ukuta na kumpatia msaada wa Tsh 200,000/= kwa ajili ya matibabu.

(vii) Kutoa misaada ya sare za Shule kwenye Vijiji vya Seka, Wanyere, Murugee na mchango wa Ada kwa Familia zisizo na uwezo.

(viii) Kuwapa pole waathirika wa kimbunga na kutoa msaada wa gharama za matibabu kwa waathirika wa mbwa mwenye kichaa katika Kijiji cha Masinono, Kata ya Bugwema.

(ix) Kutoa rambirambi katika misiba mbalimbali ya viongozi wa Chama na Serikali na wananchi wengine.

(x) Kutoa msaada wa gharama za matibabu kwa wagonjwa mbalimbali wasio na uwezo hasa wazee pale ilipowezekana.

(xi) Kutoa msaada wa gharama za kilimo kwa familia zisizo na uwezo ili kuziongezea uwezo wa kupata chakula.

(xii) Kutoa misaada ya usafiri na matengenezo ya vyombo vya usafiri kwa wazee na familia zenye watu wenye ulemavu.

(xiii) Kutoa misaada ya kujikimu kwa wazee na familia mbalimbali zisizo na uwezo.

(xiv) Kugharamia ujenzi wa nyumba ya familia ya watu wenye ulemavu wa ngozi Kijijini Kiriba.



*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (kushoto) akitoa maelekezo ya kukamilisha ujenzi wa nyumba ya kuishi familia ya Johnson Nyeura (katikati aliyeshika kinasa sauti)*



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (aliyevaa fulana ya kijani katikati) akikabidhi msaada wa mabati na saruji kwa moja ya familia zilizopatwa na maafa katika Kijiji cha Kabegi, Kata ya Ifulifu*



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo akiwa na baadhi ya Wananchi wa Vijiji vya Kata ya Ifulifu mara baada ya kuwapatia chakula cha msaada.*

## 10. KUSHIRIKIANA NA MADHEHEBU YA DINI

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amekuwa akiungana pamoja na Waumini wa Madhehebu mbalimbali wakiwemo Waislamu na Wakristu katika kuazimisha Sikukuu zao zinazotambulika kwa mujibu wa imani zao. Miongoni mwa Sikukuu hizo ni pamoja na Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan na Sikuku ya Idd El Fitr (Waislam), Pasaka na Krismasi (Wakristo)



*Waumini wa Dini ya Kiislam wakishiriki futari ya pamoja katika Msikiti wa Busekela wakati wa Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan*

Katika Sikukuu zote hizo Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini amekuwa akichangia michango mbalimbali ambayo ni pamoja na:

- Futari ya tambi, sukari, tende na mchele (Mfungo wa Ramadhan) – Waislam
- Ng'ombe kwenye sikukuu zote za kila mwaka za Idd (Waislam), Krismasi na Pasaka (Wakristo)
- Mchele, unga wa ngano, sukari, mafuta, maharage na viungo mbalimbali katika sikukuu zote za kila mwaka za Eid el Fitr, Pasaka na Krismasi



*Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wakishiriki chakula cha pamoja cha Sikukuu ya Pasaka kilichoandaliwa na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo kwenye Kanisa la Baptist Kijijini Masinono, Kata ya Bugwema*

## 11. KUWAJENGEA VIJANA UWEZO NA UJUZI

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo alifanikiwa kuwawezesha Vijana 100 kutoka Jimboni ambao walipatiwa mafunzo ya kutengeneza chaja za simu na taa zinazotumia Mionzi ya Jua. Mafunzo kwa vijana hao yalizinduliwa rasmi tarehe 20/2/2017 Kijijini Nyegina na yaliendeshwa na Dr Hong Kyu Choi kutoka Korea Kusini kwa kushirikiana na Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini. Jumla ya Vijana 100 walishiriki mafunzo na Vijana 97 walihitimu vizuri mafunzo hayo.



*Vijana wa Jimbo la Musoma Vijijini waliohitimu mafunzo ya kutengeneza chaja za simu na taa zinazotumia Mionzi ya Jua wakiwa kwenye picha ya pamoja wakati wa kufunga mafunzo hayo katika Kituo cha Nyegina, Kijijini Nyegina.*

## 12. MICHANGO YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA CHAMA

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amekuwa karibu sana na shughuli za Chama cha Mapinduzi (CCM) kuanzia ngazi ya Matawi, Kata, Wilaya, Mkoa na hata Taifa kwa ujumla. Ukaribu huu unatokana na Mbunge wa Jimbo kushiriki kwa hali na mali katika kuchangia shughuli mbalimbali za CHAMA (CCM).

## 12.1 SEKRETARIETI YA WILAYA

(i) Kununua kompyuta kwa ajili ya Ofisi ya Wilaya. Mbunge wa Jimbo amepokea ombi la kununua Printer kwa ajili ya Chama na ombi hilo litatekelezwa hivi karibuni.

(ii) Kununua vifaa vya Ofisi ngazi ya Wilaya na Jumuiya zake, Kata na Matawi.

(iii) Kununua Mashine Mbili (2) kwa Gharama ya Shilingi 1,180,000/= za kusajiria Wanachama kwa mfumo mpya wa ki-elektroniki ikiwa ni sehemu ya kuboresha na kuimarisha Chama cha Mapinduzi.

(iv) Kununua kadi 1,000 kwa kila Jumuiya (UWT, WAZAZI na UVCCM).

(v) Kutoa mafuta na posho ya kusafirisha gari la CCM Wilaya ya Musoma Vijijini kutoka Dar Es Salaam hadi Musoma.

(vi) Kuchangia posho na mafuta ya gari kwa Wajumbe wa Sekretarieti ya Wilaya katika ziara zao mbalimbali za kikazi na zile za Mbunge.

(vii) Kugharamia matengenezo na "service" za gari la Chama la Wilaya.

(viii) Kuwasaidia Wafanyakazi na viongozi wa Chama kwa shida zao za binafsi.



*Msaidizi wa Mbunge wa Jimbo Ndugu Fedson Masawa (kulia) kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, akikabidhi Kadi 1,000 kwa Katibu wa Jumuiya ya Wazazi, Musoma Vijijini, Ndugu Lucy John (katikati). Tukio hili lilishuhudiwa na Katibu wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Stephen Koyo (kushoto)*

## 12.2 MICHANGO YA VIKAO VYA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE

(i) Kutoa chakula kwa Vikao mbalimbali vya Chama, Jumuiya (Vijana na Wazazi)

(ii) Kugharamia nauli kwa Wajumbe wa Vikao vya Jumuiya za Wazazi (Mkoa), Vijana na UWT (Wilaya)

(iii) Kuchangia nauli kwa Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya kwa Vikao vyote vya kikatiba vinavyofanywa na Chama.

(iv) Kusaidia maji ya kunywa Wajumbe wote wa Kongamano la Wazazi Wilaya lililofanyika kwenye Kata ya Mugango.

(v) Kushiriki Vikao mbalimbali vya Chama na Vikao vingine kuwakilishwa na Wasaidizi wa Mbunge.



*Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Musoma Vijijini wakiwa kwenye Kikao cha Halmashauri Kuu ya Wilaya; Aliyesimama ni Ndugu Joseph Gatty aliyekuwa Katibu wa CCM Wilaya, akisisitiza Jambo kwa Wajumbe. Kulia ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya Ndugu Nyabukika Bwire Nyabukika*

## 12.3 ZIARA ZA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE

(i) Kuchangia mafuta ya Magari (usafiri na mahitaji mengine) kwa ajili ya Ziara mbalimbali za Viongozi wa CCM kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa wanapokuwa Wilayani na Mkoani.

## 12.4 CHAGUZI ZA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE

(i) Kuchangia mafuta ya Magari (usafiri) katika chaguzi za Chama ngazi ya Wilaya na Mkoa

(ii) Kuchangia nauli kwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chipukizi chini ya Jumuiya ya UVCCM kwa ajili ya Uchaguzi wa Viongozi wao.



*Wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mara wakiendelea na zoezi la kupiga kura katika Uchaguzi wa Chama ngazi ya Mkoa ambao Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo alichangia Mafuta ya Magari ili kufanikisha uchaguzi huo na nyingine za Wilaya*

## 12.5. SHEREHE ZA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE

(i) Kuchangia Mabati 54 kwa ajili ya Shule ya Msingi Kiriba wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ikiwa ni uamuzi wa kuunga mkono jitihada za Wanawake.

(ii) Kununua Miche ya Miti ili kuungana na Jumuiya ya WAZAZI katika kuadhimisha Sherehe za Wiki ya Wazazi ki-Mkoa zilizofanyika Kijijini Maneke. Hii ilikuwa ni sehemu ya kampeni ya Utunzaji wa Mazingira.

(iii) Kushiriki Sherehe za Wiki ya Wazazi ki- Mkoa Kijijini Maneke. Mbunge wa Jimbo alikuwa Mgeni Rasmi.

(iv) Kugharimia vyakula kwa ajili ya Sherehe za Wiki ya Wazazi Mkoa iliyofanyika Kijijini Maneke.

(v) Kugharamia nauli kwa Viongozi na Watendaji wa Mkoa na Wilaya katika sherehe za Wiki ya Wazazi Mkoa wa Mara.

(vi) Kushawishi akina Mama na Vijana wa CCM kuunda Vikundi vya uzalishaji kwa ajili ya kupewa Mikopo ili vijitegemee ki-uchumi.




*Viongozi mbalimbali na Wajumbe wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Mara wakiwa kwenye picha ya pamoja na Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo (wa pili aliyesimama kulia) kwenye Maadhimisho ya Sherehe za Wiki ya Wazazi ki-Mkoa zilizofanyika tarehe 29/03/2018 Kijijini Maneke, Kata ya Busambara*



*Msaidizi wa Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Ndugu James Francis (kushoto) akikabidhi jumla ya Mabati 54 kwa Jumuiya ya Wanawake kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, kwa ajili ya kuezeka chumba kimoja cha darasa katika Shule ya Msingi Bwai Kumusoma*

## 13. WAZALIWA WA VIJIJI VYA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Kwa kipindi chote cha Miaka Mitatu na Nusu, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amewaunganisha Wazaliwa wa Vijiji vya Jimbo hili waishio ndani na nje ya Musoma Vijijini, ili kushiriki katika shughuli za Uchangiaji wa Miradi ya Maendeleo kwenye maeneo walikozaliwa kama ifuatavyo:

### (i) Ujenzi wa Zahanati

Miongoni mwa Wadau wa Maendeleo na Wazaliwa waliojitokeza na kushiriki katika ujenzi huu ni wale waliochangia ujenzi wa Zahanati za Mkirira, Kigera Etuma, Mwiringo na Chimati. Mbunge wa Jimbo ametoa michango mikubwa kwenye ujenzi wa Zahanati hizi.

**(ii) Vituo vya Afya**

Kituo cha Afya cha Kata ya Nyambono ni Kituo kinachojengwa kwa kutumia michango ya Wazaliwa wa Kata ya Nyambono wanaoshirikiana na ndugu zao wa Vijijini. Mbunge wa Jimbo ametoa mchango mkubwa kwenye ujenzi wa Kituo hiki.

**(iii) Ujenzi wa Shule za Msingi na Sekondari**

Wazaliwa wa Jimbo la Musoma Vijijini wameendelea kuungana na Mbunge wa Jimbo kuchangia ujenzi wa Shule za Msingi na Sekondari. Shule za Sekondari zinazojengwa kwa kutumia michango ya Wazaliwa hawa ni Dan Mapigano Memorial Secondary School (Kata ya Bugoji), Busamba Sekondari (Busambara), Sekondari Mpya ya Nyegina (Nyegina) na Sekondari Mpya ya Kigera (Nyakatende). Vilevile kuna ujenzi wa Shule za Msingi zikiwemo Kanyega (Murangi) na Shule ya Msingi Chimati (Makojo). Mbunge wa Jmbo anachangia ujenzi wa mashule haya.

**(iv) Walimu wa Kujitolea**

Kwa kuguswa na Jitihada anazozifanya Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, Wazaliwa wa Musoma Vijijini wameungana nae kwa kuchangia Mradi wa Walimu wa Kujitolea katika Sekondari za Kata zao na Kata za Jirani. Posho za Walimu wa Kujitolea katika Sekondari za Kata ya Bukima, Busambara na Suguti zimepatikana. Orodha kamili ya wachangiaji hawa wote inapatikana kwenye Ofisi ya Mbunge wa Jimbo. Mbunge wa Jimbo anachangia Posho za Walimu wa Kujitolea wa Sekondari 4 kwa miaka miwili (2019 - 2021).

**(v) Mazingira**

Wadau wa Maendeleo kupitia kikundi cha Nyanja Development Initiative (NDI), wameungana na Wabunge wa Jimbo la Musoma Vijijini na Musoma Mjini, na Mkuu wa Wilaya ya Musoma katika kuanzisha na kuendeleza Mradi wa kuotesha miche ya miti. Huu ni Mradi wa miche zaidi ya Milioni 10.

## 14. KUJADILI NA KUTATHMINI MAENDELEO YA JIMBO

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo amejiwekea utaratibu wa kukutana na Wananchi, Wadau mbalimbali wa Maendeleo ya Jimbo kila mwisho wa mwaka ili kujadili na kutathimini shughuli na mwenendo mzima wa Maendeleo ya Jimbo.

Ili kufanikisha Mkutano huu mkubwa, Mbunge wa Jimbo, amekuwa akigharamia kila kitu ikiwemo nauli kwa Wajumbe Maalum (Wawakilishi kutoka Vijijini). Huu ni mpango endelevu kwa Maendeleo ya Jimbo.

Mbali na utaraibu huo aliojiwekea, Mbunge wa Jimbo, ameunda Mabaraza ya Wazee ya Ushauri, Ushawishi, Utamaduni na Maadili ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini ambayo kazi yao kuu ni kushawishi na kushauri mambo yanayohusu shughuli za Maendeleo

kwenye Vijiji vyao na Kata zao bila kuingilia wala kuwa na mamlaka ya uongozi. Mabaraza haya yanakutana mara mbili kwa mwaka kufanya tathimini ya Maendeleo kwenye Vijiji vyao na Kata zao.



*Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wazee kutoka kwenye vijiji mbalimbali ambao walikutana kwenye Kijiji cha Murangi na kuunda Baraza la Jimbo la Wazee wa Musoma Vijijini*

## 15 HITIMISHO

Jimbo la Musoma Vijijini lenye Vitongoji 374, Vijiji 68 na Kata 21 lina Kaya takribani 52,830. Jimbo hili linatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 – 2020 kwa MAFANIKIO MAKUBWA SANA.

MAFANIKIO makubwa haya yanatokana na WANANCHI VIJIJINI kukubali KUJITOLEA kutekeleza MIRADI ya MAENDELEO iliyobuniwa na kuasisiwa na wao wenyewe wakishirikiana na SERIKALI yao.

AHADI ZOTE za Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt John Joseph Pombe Magufuli alizotoa kwa Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini ZINATEKELEZWA kwa kasi kubwa ikiwemo ya ujenzi wa kiwango cha LAMI barabara ya Musoma – Mugango – Makojo – Busekela. AHADI nyingine za Viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali wa ngazi mbalimbali nazo zinatekelezwa kwa kasi ya kuridhisha.

AHADI zote hizi zinatoka kwenye Andiko la Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 – 2020. Kwahiyo, MIRADI ya MAENDELEO ya Jimbo la Musoma Vijijini kwenye Sekta za ELIMU, AFYA, KILIMO (Ufugaji na Uvuvi), MAZINGIRA, MICHEZO na UTAMADUNI, imetayarishwa na kutekelezwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020). MIRADI ya USAMBAZAJI wa UMEME na MAJI Vijijini nayo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani hii ya CCM. Hivyo ndivyo ilivyo kwa MIRADI ya USAFIRISHAJI na MAWASILIANO inayotekelezwa ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo ANASHIRIKIANA vizuri SANA na Wananchi Vijijini, Viongozi wa Chama na Serikali wa ngazi zote KUTEKELEZA kwa MAFANIKIO MAKUBWA Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020). Mbunge huyu wa Jimbo la Musoma Vijijini AMETOA MICHANGO MINGI na MIKUBWA kwenye MIRADI YOTE ya Maendeleo kwenye Vijiji Vyote 68 na Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini. AHADI za Mbunge wa Jimbo zimetekelezwa na KUVUKA malengo yaliyowekwa hapo awali.

## 16. SHUKRANI

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anatoa shukrani nyingi kwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe Dkt Ali Mohamed Shein, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Mhe Philipo Mangula na Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Dkt Bashiru Ally kwa usimamizi wao thabiti wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2015 – 2020.

Mbunge wa Jimbo, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini anatoa shukrani nyingi kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Mhe Kasim Majaliwa Kasim, Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Viongozi wote wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa katika kuunga mkono jitihada za Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kutekeleza Vipaumbele vyao vya Afya, Elimu, Kilimo (na Ufugaji na Uvuvi),

Mazingira, Michezo na Utamaduni ambavyo vimo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 - 2020.

Vilevile, Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanatoa SHUKRANI nyingi kwa SERIKALI yao inayotekeleza MIRADI ya upatikanaji wa MAJI na UMEME Vijijini mwao. Miradi ya Miundombinu ya USAFIRISHAJI na MAWASILIANO nayo inatekelezwa Vijijini mwao ikiwa ni sehemu muhimu ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 – 2020).

Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anamshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Mara, Mhe Adam Malima na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Mhe Dr Vincent Naano Anney kwa jitihada na ushirikiano mzuri wanaoutoa kwenye utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwenye Vijiji vyote 68 na Kata zote 21 za Jimbo la Musoma Vijijini.

Shukrani nyingi zinatolewa kwa Uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Jumuiya zake kwa ngazi zote tokea Tawi, Wilaya hadi Mkoa. Shukrani za kipekee zinatolewa kwa Mlezi wetu ki-chama (CCM) wa Mkoa, Ndugu Kheri James, Mwenyekiti wa CCM Mkoa Ndugu Samweli Kiboye, Katibu wa CCM Mkoa wa Mara Ndugu Shaibu Ngatiche, MNEC Mkoa wa Mara Ndugu Christopher Gachuma, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Nyabukika Bwire Nyabukika, Katibu wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Stephen Koyo, na Viongozi wengine wote wa CCM na Jumuiya zake ngazi ya Wilaya na Mkoa.

Shukrani zinatolewa pia kwa Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma wakiongozwa na Mwenyekiti

wa Halmashauri hiyo Mhe Charles Magoma, kwa kusimamia vizuri Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa kwenye Kata zao. Madiwani hawa wanatoa ushirikiano mzuri sana kwa Mbunge wa Jimbo na Wasaidizi wake watatu (Ndugu Fedson Masawa, Hamisa Gamba na Verediana Mgoma).

Aidha, Mbunge wa Jimbo, anatoa shukrani nyingi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Musoma, Ndugu John Lipesi Kayombo, Wakuu wote wa Idara za Halmashauri ya Musoma (Musoma DC), Watendaji wote ngazi ya Kata na Vijiji kwa jitihada zao za usimamiaji mzuri wa Miradi ya Maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini. Wafanyakazi wote wa Halmashauri yetu wanapewa shukrani za dhati kwa kutimiza wajibu wao wenye mafanikio mazuri.

Mbunge wa Jimbo, anawashukuru Ndugu Isack Kambira Mtendaji Mkuu wa Tovuti ya Jimbo la Musoma Vijijini kuhakikisha taarifa za maendeleo ya Jimbo zinawafikia Wananchi ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini, Mkoa, Taifa na Ulimwenguni kote. Ndugu Kingi Imani na Ndugu Riadha Saidi wanapewa shukrani kwa kusambaza taarifa za Maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini kupitia Redio ya Mtandaoni inayojulikana kwa jina la “Musoma Vijijini Online Redio”

Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo anawashukuru Wadau mbalimbali wa Maendeleo, kwa kutambua michango yao wanayoendelea kutoa ili kufanikisha Miradi ya Maendeleo ya Sekta mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na: NMB, PCI, EP4R, EQUIP, BMZ, Madhehebu ya Dini na Wazaliwa wa Jimbo la Musoma Vijijini waishio ndani na nje ya Jimbo. Serikali za Australia, China, Japan, Korea Kusini, Ujerumani, Uingereza na Marekani zinatambuliwa kwa Misaada yao kwa Jimbo letu.

Shukrani za pekee kabisa ziwaendee WANANCHI WOTE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Kata zote 21, Vijiji 68 na Vitongoji vyote 374 kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa katika kujitolea kuchangia shughuli mbalimbali za Maendeleo ndani ya Jimbo letu. Wazee wa Mabaraza ya Ushauri, Ushawishi, Utamaduni na Maadili ya Kata zote 21 na Vijiji 68 wanapewa shukrani nyingi kwa kushawishi na kuhimiza kwa MAFANIKIO ya KUJIVUNIA ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (2015 – 2020) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

**KIAMBATANISHO NAMBA I**

Orodha ya baadhi ya ziara za Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo alizofanya kwa kipindi cha Januari 2016 – Juni 2019. Mbunge wa Jimbo ametembelea Vijiji vyote 68 na Kata zote 21 kwa zaidi ya mara 3 – 5

| Na | TAREHE | MAHALI | SHUGHULI | MCHANGO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 23/12/2015 | Murangi | Kupanga Mipango ya Maendeleo ya Jimbo | Chakula |
| 2 | 22/01/2016 | Mkirira | Kugawa Vitabu vya Sayansi na Kiingereza | Vitabu |
| 3 | 04/03/2016 | Murangi | Kukabidhi Ambulance kubwa Kituo-Murangi | Usafiri |
| | | | Kuchangia ukamilishaji wodi ya akina mama | Bati 50 & Saruji 400 |
| 4 | 06/03/2016 | Murangi | Kuwatambulisha Madaktari kutoka China | Kuleta Madaktari |
| 5 | 07/03/2016 | Ekungu | Kuzungumza na wananchi wa Ekungu | ……. |
| | | Seka | Kuzungumza na wananchi wa Kijiji cha Seka | …….. |
| | | Kataryo | Kuzungumza na wananchi wa Kijiji Kataryo | ……. |
| 6 | 10/03/2016 | Murangi | Kusaini Msaada wa Milioni 170 uliotolewa na Serikali ya Japan kusaidia Mradi wa upanuzi wa Kituo cha Afya cha Murangi | Wadau wa Maendeleo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7 | 06/05/2016 | Suguti | Kuhidhinisha M/fedha za mfuko wa Jimbo | Usafiri |
| 8 | 07/05/2016 | Rukuba | Kuzindua zoezi la ugawaji madawati | Madawati 100 |
| | | | | Saruji 100 |
| | | Saragana | Kuzindua Tovuti ya Jimbo Kijijini Saragana | ------ |
| 9 | 25/06/2016 | Mugango | Kuwatambulisha Madaktari Bingwa | ……. |
| | | Kwibara | Kugawa Vitabu vya Sayansi na Kiingereza | Vitabu |
| | | Kigera Etuma | Kusherehekea siku ya kuzaliwa kwake | Chakula |
| 10 | 26/06/2016 | Bukumi | Kukabidhi Madawati S/M Bukumi | Madawati 71 |
| | | | Kuchangia ujenzi wa darasa 1 na Nyumba 1 | Saruji mifuko 59 |
| | | | | Mabati 100 |
| | | Kwibara | Kukabidhi Madawati S/M Kwibara A&B | Madawati 97 |
| | | Nyasurura | Kukabidhi Madawati S/M Nyasurura | Madawati 73 |
| | | | | Saruji mifuko 100 |
| | | | Harambee ujenzi wa S/M Nyasurura | Mabati 100 |
| 11 | 21/07/2016 | Masinono | Kukabidhi Gari la wagonjwa - Zahanati | Gari 1 la wagonjwa |
| | | Buraga | Kukabidhi Gari la | Gari 1 la |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wagonjwa - Zahanati | wagonjwa |
| | | | Harambee ujenzi wa nyumba ya Mganga 2/1 | Saruji mifuko 50 |
| 12 | 22/07/2016 | Mugango | Kukabidhi Gari la wagonjwa - Zahanati | Gari 1 la wagonjwa |
| | | | Harambee ujenzi wa wadi ya mama na mtoto | Saruji mifuko 400 |
| | | Nyakatende | Kukabidhi Gari la wagonjwa - Zahanati | Ambulance 1 |
| | | Nyasurura | Madaktari Bingwa Zahanati ya Nyakatende | Kuleta Madaktari |
| 13 | 07/08/2016 | Suguti | Mashindano ya kwaya sherehe za Nanenane | Usafiri, Zawadi & Chakula |
| 14 | 08/08/2016 | Suguti | Mashindano ya ngoma sherehe za Nanenane | Usafiri, Zawadi, Chakula |
| | | | Harambee vyumba vya madarasa S/M Suguti | Saruji mifuko 100 |
| 15 | 20/09/2016 | U/ Mkendo | Kugawa vitabu kwa Wabunge wote wa Mara | Vitabu |
| 16 | 03/10/2016 | Murangi | Kukabidhi vitanda Hospital ya Murangi | Vitanda & Chakula |
| 17 | 25/11/2016 | Kabegi | Kuwapa pole waathirika wa kimbunga | Mabati Saruji & Misumali |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Bukima | Kumpa pole mama mjane kutokana na athari ya kimbunga | Mabati, Saruji, Misumari & Mbao |
| 18 | 23/12/2016 | Murangi | Kikao cha Tathimini ya Maendeleo ya Jimbo | Chakula & Nauli |
| 19 | 25/12/2016 | Kamguruki | Kushiriki Ibada katika Kanisa la Menonite | Chakula |
| | | | Kikao cha uhamasishaji wa maendeleo | |
| | | | Kushiriki chakula cha Christmas na wananchi | |
| 20 | 26/12/2016 | Tegeruka | Kuidhinisha fedha za Mfuko wa Jimbo | Usimamizi |
| 21 | 31/12/2016 | Etaro | Mashindano ya kupiga kasia | Zawadi & Usafiri wa Vikundi |
| | | Etaro S/M | Kugawa vitabu kwa shule zenye Maktaba | Vitabu |
| 22 | 20/02/2017 | Nyegina | Kuzindua mafunzo ya taa na chaja kwa vijana | Gharama za Mafunzo |
| | | Kome | Kukagua ujenzi wa madarasa S/M Kome B | ……. |
| 23 | 24/02/2017 | Seka | Kuzungumza na wananchi (tukio la wizi) | ……….. |
| 24 | 15/04/2017 | Bugoji | Ujenzi wa madarasa S/M Kanderema “B” | ………. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Muhoji | Ujenzi wa madarasa S/M Muhoji | ……. |
| | | Masinono | Harambee ya ujenzi wa choo cha zahanati | Nondo, Wavu, na Masink |
| | | Chumwi | Kuaga mwili wa Mwalimu S/M Chumwi | ….. |
| 25 | 16/04/2017 | Mwiringo | Kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa | ……. |
| | | B. Kumusoma | Kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa | Saruji mifuko 50 |
| | | Kiriba | Chakula cha Pasaka na wananchi | Chakula |
| 26 | 07/05/2017 | Saragana | Kuwatambulisha madaktari kutoka china | Madaktari |
| | | Musanja | Kuwapa pole waathirika wa kimbunga | …….. |
| | | Bulinga | Kukagua ujenzi vyumba vya madarasa | ………. |
| 27 | 31/08/2017 | Murangi | Kuzindua nyumba ya Mganga Afya/Murangi | …….. |
| 28 | 13/11/2017 | Nyasurura | Kuhidhinisha M/fedha za Mfuko wa Jimbo | Usimamizi |
| 29 | 19/11/2017 | Rusoli | Kuwapa pole waathirika wa Mafuriko | ………. |
| | | Bukumi | Kuwapa pole waathirika wa Kimbunga | ………… |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Busekera | Kuwapa pole waathirika wa Kimbunga | Gharama za Matibabu Mzee 1 |
| | | Kastam | Kuwapa pole waathirika wa Mafuriko | ………. |
| 30 | 20/11/2017 | Mabui | Kuwapa pole waathirika wa Kimbunga | …….. |
| | | Seka | Kuwapa pole waathirika wa Kimbunga | Sare na Vifaa vya Shule familia 1 |
| | | Kurukerege | Kuwapa pole waathirika wa Kimbunga | 200,000/= Mjamzito |
| 31 | 25/12/2017 | Nyambono | Kushiriki misa ya Chrismass K. Menonite | Chakula |
| | | | Kushiriki chakula cha pasaka na wananchi | |
| | | | Jiwe la Msingi ujenzi wa Kituo cha Afya | |
| 32 | 29/12/2017 | Bukima | Ujenzi vyumba vya madarasa na Zahanati | …….. |
| | | Kasoma | Ujenzi wa Vyumba vya madarasa | ……. |
| | | Nyasaungu | Ujenzi wa Zahanati na Madarasa | …….. |
| 33 | 23/01/2018 | Murangi | Kuidhinisha M/fedha za Mfuko wa Jimbo | Usimamizi, Chakula na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Kukutana na wawakilishi wa wazee kata | Nauli |
| 34 | 15/01/2018 | Murangi | Kushiriki ziara ya Waziri mkuu – Musoma V. | …… |
| 35 | 12/02/2018 | Mwiringo | Kuchangia ukamilishaji wa zahanati | Samani zote & Gharama za Fundi |
| 36 | 15/02/2018 | Nyasaungu | Kushiriki Harambee ujenzi wa zahanati | Saruji mifuko 100 |
| 37 | 15/03/2018 | Burungu | Kuwapa pole waathirika wa Kimbunga | Chakula - Waathirika |
| | | Bukumi | Kuitembelea S/M Bukumi iliyoezuliwa | Chakula - Waathirika |
| | | Busekera | Kuwapa pole waathirika wa kimbunga | …….. |
| | | Bugwema | Kuwapa pole waathirika wa kimbunga na waathirika wa Mbwa wenye Kichaa | Matibabu |
| 38 | 20/02/2018 | Musoma (M) | Kuhudhuria kikao cha Baraza la Madiwani | ………. |
| 39 | 21/02/2018 | Mkirira | Kugawa Mbegu za Alizeti na Ufuta Bure | Alizeti na Ufuta |
| | | Tegeruka | Kugawa Mbegu za | Alizeti na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Alizeti na Ufuta Bure | Ufuta |
| | | Suguti | Kugawa Mbegu za Alizeti na Ufuta Bure | Alizeti na Ufuta |
| | | Masinono | Kugawa Mbegu za Alizeti na Ufuta Bure | Alizeti na Ufuta |
| | | Busungu | Kugawa Mbegu za Alizeti na Ufuta Bure | Alizeti na Ufuta |
| 40 | 16/03/2018 | B. Kumusoma | Kuipa pole familia iliyoangukiwa na nyumba | Chakula - Mfiwa |
| | | Kurukerege | Kuwapa pole waathirika wa kimbunga | ……….. |
| | | Mkirira | Kuwapa pole waathirika wa kimbunga | ……… |
| 41 | 29/03/2018 | Maneke | Mgeni rasmi Sherehe za wiki ya Wazazi Mkoa wa Mara | Gharama za Miche na Chakula |
| 42 | 01/04/2018 | Masinono | Kushiriki Ibada ya pasaka Kanisa la Baptist | Zawadi - Kwaya |
| | | | Chakula cha Pasaka pamoja na wananchi | Chakula |
| 43 | 28/04/2018 | Nyamrandirira | Mazishi ya Mbunge Magoti Chinuno | Gharama za Msiba |
| 44 | 30/04/2018 | Chumwi | Uzinduzi mabaraza Wazee wa ushauri Kata | Nauli kwa Wajumbe |
| | 01/05/2018 | Kurwaki | Harambee ya ujenzi wa | Saruji 350 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 45 | | | Zahanati ya kijiji | na fundi |
| | | Kigera Etuma | Harambee ya ujenzi wa Zahanati ya kijiji | Saruji mifuko 50 |
| 46 | 02/05/2018 | Mkirira | Harambee ya ujenzi wa Zahanati | Saruji mifuko 200 |
| 47 | 13/06/2018 | Bukima | Harambee ya ujenzi wadi la mama na mtoto | Saruji mifuko 100 |
| | | Saragana | Harambee ya ujenzi wa kituo cha Polisi | Saruji mifuko 100 |
| | | Nyambono | Harambee ujenzi wa Kituo cha Afya | Saruji mifuko 100 |
| 48 | 15/06/2018 | Nyakatende | Kujumuika na waumini wa Kiislamu (Idd) | Chakula |
| | | Kwikuba | Kukagua Eneo/Mradi wa ujenzi wa Sekondari | Chakula |
| | | | Kujumuika na waumini wa Kiislamu (Idd) | |
| | | Kasoma | Kujumuika na waumini wa Kiislamu (Idd) | Chakula |
| 49 | 16/06/2018 | Mkirira | Kukagua Mradi wa Ujenzi wa Zahanati | …….. |
| | | Nyasaungu | Kukagua Mradi wa Ujenzi wa Zahanati | ……… |
| | | Kurwaki | Kukagua Mradi wa Ujenzi wa Zahanati | Saruji mifuko 100 |
| 50 | 10/07/2018 | Halmashauri | Kushiriki kikao na wataalama na wadau wa kilimo | Ushauri |
| 51 | 11/07/2018 | CCM | Kushiriki kikao cha | ……….. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Wilaya | K/Siasa CCM Wilaya | |
| 52 | 12/07/2018 | CCM Mkoa | Kushiriki kikao cha H/Kuu Mkoa | …….. |
| 53 | 13/07/2018 | Murangi - RK | Kushiriki kikao cha H/kuu CCM Wilaya | Nauli kwa Wajumbe |
| 54 | 15/07/2018 | Nyegina | Uzinduzi wa Shule ya Msingi Nyegina B | Saruji mifuko 50 |
| 55 | 16/07/2018 | Kwibara | Kikao na walimu wakuu S/M 112 na MEKs | Nauli kwa Wajumbe |
| 56 | 04/08/2018 | Chumwi | Kushiriki Kikao cha H/kuu CCM Wilaya | Nauli kwa Wajumbe |
| 57 | 06/08/2018 | Makojo Sekondari | Kikao cha Maendeleo ya Elimu na Wakuu wa Sekondari 20 MEKs | Nauli kwa Wajumbe |
| 58 | 08/08/2018 | Musoma (M) | Kukabidhi SIMTANK – Mradi wa miche | SIMTANK |
| | | Nyegina | Kukabidhi vitabu Nyegina S/M & Sekondari | Vitabu |
| 59 | 10/08/2018 | Suguti | Kikao na Wataalamu wa Kilimo | Nauli kwa Wajumbe |
| 60 | 30/08/2018 | Kanderema | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Bugoji | Mbegu Kg 300 |
| | | Muhoji | Kugawa Mbegu Vijiji vya Kata ya Bugwema | Kg 400 |
| | | Nyabaenger e | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Musanja | Kg 300 |
| | | Lyasembe | Kugawa Mbegu Vijiji | Kg 200 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vya Kata ya Murangi | |
| | | Kwikerege | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Rusoli | Kg 300 |
| 61 | 31/08/2018 | Butata | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Buukima | Kg 300 |
| | | Bujaga | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Bulinga | Kg 300 |
| | | Bwasi | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Bwasi | Kg 300 |
| | | Chimati | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Makojo | Kg 300 |
| | | Buira | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Bukumii | Kg 400 |
| 62 | 01/08/2018 | Chirorwe | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Suguti | Kg 400 |
| | | Nyambono | Kugawa Mbegu Vijiji vya Kata ya Nyambono | Kg 200 |
| | | Mikuyu | Kugawa Mbegu Kata ya Nyamrandirira | Kg 500 |
| | | Mwiringo | Kugawa Mbegu Vijiji vya Kata ya Busambara | Kg 300 |
| | | Kiriba | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Kiriba | Kg 300 |
| 63 | 02/08/2018 | Kataryo | Kugawa Mbegu Vijiji vya Kata ya Tegeruka | Kg 300 |
| | | Nyang’oma | Kugawa Mbegu Vijiji vya Kata ya Mugango | Kg 300 |
| | | Kiemba | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Ifulifu | Kg 300 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kakisheri | Kugawa Mbegu Vijiji vya Kata Nyakatende | Kg 400 |
| | | Kurukerege | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Nyegina | Kg 300 |
| | | Mmahare | Kugawa Mbegu Vijiji vyote Kata ya Etaro | Kg 400 |
| 64 | 04/08/2018 | Kisorya | Kushiriki Ziara ya Rais Wilayani Bunda | ……… |
| 65 | 05/08/2018 | Musoma (M) | Kushiriki Ziara ya Rais Wilayani Musoma | ………. |
| 66 | 09/10/2018 | Buanga | Kushiriki Harambee ujenzi wa S/M Mpya | Saruji mifuko 100 |
| | | Butata | Kushiriki Harambee ujenzi wa Zahanati | Saruji mifuko 50 |
| | | Mmahare | Kushiriki Harambee ujenzi wa Zahanati | Saruji mifuko 50 |
| | | Suguti | Kukutana na Wasaidizi wa Kisheria | ……… |
| 67 | 10/10/2018 | Maneke | Kikao cha Baraza la wazee ngazi ya Vijiji | Usafiri & Chakula |
| 68 | 11/10/2018 | Musoma | Kushiriki kikao cha DCC Musoma | ……… |
| 69 | 12/10/2018 | Nyasurura | Kikao cha Baraza la wazee ngazi ya Kata | Usafiri & Chakula |
| 70 | 17/10/2018 | Musoma | Kushiriki kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa | …… |
| 71 | 14/12/2018 | Chitare | Kukagua ujenzi wa shule shikizi ya Mwikoko | Saruji mifuko 50 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Makojo | Kukagua Miradi na Kuongea na wananchi | …… |
| | | Chimati | Kukagua ujenzi wa Zahanati | Saruji mifuko 50 |
| | | Busungu | Kukagua ujenzi wa madarasa | Saruji mifuko 50 |
| | | Bulinga | Ujenzi wa Madarasa na Maabara Bulinga Sec | Saruji mifuko 50 |
| | | Bujaga | Kukagua Ujenzi wa Madarasa Kurugongo B | Saruji mifuko 50 |
| 72 | 15/12/2018 | Kiriba | Kuzungumza na wananchi na kukagua Miradi | …… |
| | | B. Kumusoma | Kuongea na Wananchi | …… |
| | | B. Kwitururu | Kukagua ujenzi wa madarasa S/M Chanyauru | Mabati 52 |
| | | | Kukagua ujenzi wa zahanati | …… |
| | | Mwiringo | Kukagua ujenzi wa madarasa | …… |
| | | Kwikuba | Kukagua ujenzi wa sekondari ya Busambara | Mabati 96 |
| | | Maneke | Kukagua ujenzi wa Zahanati | …… |
| 73 | 17/12/2018 | Maneke | Kikao cha Wataalam | Nauli |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wa Kilimo cha Muhogo | |
| 74 | 18/12/2018 | Musoma (M) | Kikao cha K.Siasa CCM Wilaya Musoma (V) | …… |
| 75 | 19/12/2018 | Murangi | Kikao cha H.Kuu ya CCM Wilaya Musoma V | Nauli kwa Wajumbe |
| 76 | 20/12/2018 | Masinono | Kukagua ujenzi wa madarasa S/M Masinono | Mabati 151 |
| | | Muhoji | Kukagua ujenzi wa madarasa na zahanati | …… |
| | | Nyasaungu | Kukagua ujenzi wa Zahanati | …… |
| | | Kiemba | Kukagua ujenzi wa Madarasa | …… |
| | | Kabegi | Kukagua ujenzi wa shule shikizi Binyago | Saruji mifuko 50 |
| 77 | 21/12/2018 | Bukumi | Kukagua ujenzi wa zahanati Burungu | Saruji mifuko 50 |
| | | Busekera | Kukagua ujenzi wa Maabara Mtiro Sekondari | Mabati 55 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Kukagua Ujenzi wa Madarasa S/M Buesekera | Mabati 40 |
| | | Buira | Kukagua Ujenzi wa Madarasa S/M Buira | Mabati 54 |
| | | Buraga | Kukagua ujenzi wa Madarasa S/M Buraga | …… |
| | | | Ujenzi wa shule shikizi Buraga Mwaloni | Saruji mifuko 50 |
| | | Kwikerege | Kuzungumza na Wananchi | …… |
| | | Rusoli | Ujenzi wa madarasa S/M Rusoli A&B | Mabati 50 |
| | | Buanga | Kukagua ujenzi wa Shule mpya Buanga | Saruji mifuko 50 |
| 78 | 22/12/2018 | Kaburabura | Kuzungumza na wananchi | …… |
| | | Bugoji | Kukagua ujenzi wa Sekondari ya Bugoji | Saruji mifuko 175 |
| | | Saragana | Kuzungumza na Wananchi | …… |
| | | Nyambono | Kukagua ujenzi wa Kituo cha Afya | Nondo 18 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 79 | 24/12/2018 | Kurwaki | Harambee uezekaji wa Zahanati | Mabati Bando 144 |
| | | Nyang'oma | Kukagua ujenzi wa Kituo cha Afya | …… |
| | | Kwibara | Ukamilishaji wa Maabara Mugango Sek | Saruji mifuko 50 |
| | | Mkirira | Kukagua ujenzi wa zahanati | …… |
| | | Nyegina | Kukagua ujenzi wa madarasa S/M Nyegina B | …… |
| | | Kurukerege | Kukagua ujenzi wa madarasa S/M Bukwaya | Mabati 65 |
| | | | Ujenzi wa Zahanati Kurukerege | …… |
| 80 | 25/12/2018 | Bukima | Ujenzi wa Maabara Parokia ya Bukima | Saruji mifuko 50 |
| | | Bukumi | Sikukuu ya Chrismas kanisa la RC Bukumi | Chakula |
| 81 | 31/12/2018 | B. Kwitururu | Chakula cha Pamoja cha kufunga mwaka | Chakula |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 82 | 04/01/2019 | Musoma (M) | Kushiriki Kikao cha Halmashauri Kuu Mkoa | …… |
| 83 | 05/01/2019 | Mikuyu | Kukagua ujenzi wa Madarasa S/M Mikuyu | Mabati 54 |
| | | Chumwi | Kukagua ujenzi wa vyumba vya Madarasa | ….. |
| | | Seka | Kukagua ujenzi wa Madarasa Nyamurandirira | ….. |
| | | | Kukagua ujenzi wa Madarasa S/M Seka B | Saruji mifuko 50 |
| | | Kasoma | Kutembelea Shule ya Kasoma Sekondari | ….. |
| | | | Kukagua ujenzi wa madarasa Kasoma S/M | ….. |
| | | | Harambee ujenzi wa madarasa S/M Rwanga | Mabati 150 |
| | | | | Saruji mifuko 50 |
| | | K. Etuma | Kukagua ujenzi wa | Mabati 90 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Madarasa S/M Kigera | |
| | | Kakisheri | Ujenzi wa Zahanati | ….. |
| | | Nyakatende | Ujenzi wa Madarasa S/M Nyakatende | ….. |
| | | | Ujenzi wa Madarasa Nyakatende Sekondari | Saruji mifuko 50 |
| | | | Ujenzi wa Madarasa Nyakatende Sekondari | Mabati 58 |
| 84 | 06/01/2018 | Bwasi | Ujenzi wa Madarasa S/M Bwasi B | Saruji mifuko 10 |
| | | Kome | Ukamilishaji wa Maabara Nyanja Sekondari | Saruji mifuko 50 |
| | | | Kuezeka Madarasa S/M Kome B | Mabati 72 |
| | | Bugunda | Ujenzi wa Madarasa S/M Bulinga A&B | ….. |
| | | Bukima | Ujenzi wa Madarasa S/M Bukima Sekondari | Saruji mifuko 100 |
| | | | | Mabati 58 |
| | | Kastam | Ujenzi wa Madarasa | Saruji |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | S/M Mkapa | mifuko 50 |
| 85 | 07/01/2019 | Mabui | Ujenzi wa Madarasa Mabui Sekondari | ….. |
| | | Musanja | Ujenzi wa Shule mpya Gomola | Saruji mifuko 50 |
| | | Nyabaengere | Ujenzi wa Madarasa S/M Nyabaengere | Mabati 108 |
| | | Lyasembe | Ujenzi wa Madarasa S/M Murangi | ….. |
| | | Murangi | Ujenzi wa Madarasa Murangi Sekondari | Saruji mifuko 50 |
| 86 | 08/01/2019 | Wanyere | Ujenzi wa Madarasa S/M Murugee | Saruji mifuko 50 |
| | | | Ujenzi wa Madarasa S/M Wanyere A | Saruji mifuko 25 |
| | | | Ujenzi wa Madarasa S/M Wanyere B | Mabati 50 |
| | | | | Saruji mifuko 25 |
| | | Chirorwe | Kukagua ujenzi wa Zahanati | ….. |
| | | Kusenyi | Ujenzi wa Madarasa S/M Kusenyi A | Mabati 54 |
| | | | | Saruji mifuko 20 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Suguti | Ujenzi wa Madarasa S/M Suguti A | Saruji mifuko 50 |
| | | | Ujenzi wa Madarasa S/M Suguti B | Saruji mifuko 50 |
| 87 | 09/01/2019 | Kataryo | Ujenzi wa Madarasa S/M Kataryo | Mabati 54 |
| | | Mayani | Ujenzi wa Madarasa Tegeruka Sekondari | Mabati 54 |
| | | Tegeruka | Ujenzi wa Madarasa S/M Nyaminya | Mabati 54 |
| | | Busamba | Ujenzi wa Madarasa S/M Egenge | Saruji mifuko 50 |
| | | Etaro | Ujenzi wa Madarasa S/M Etaro | Mabati 144 |
| 88 | 11/01/2019 | Rukuba | Ujenzi wa Maktaba S/M Rukuba | Mabati 57 |
| 89 | 21/04/2019 | Rukuba | Uzinduzi wa Maktaba S/M Rukuba | Kibao cha Uzinduzi |
| | | | Kushiriki Chakula cha Mchana cha Pasaka | Chakula |
| 90 | 22/04/2019 | Bugoji | Jiwe la Msingi Dan Mapigano Sekondari | Kibao na Chakula |
| | | | | Kibao Jiwe |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | la Msingi |
| 91 | 31/05/2019 | Musoma V | Kushiriki Mbio za Mwenge | Ng’ombe (Mboga) |
| 92 | 31/05/2019 | Kakisheri | Kukagua Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Kakisheri | Saruji mifuko 50 |

**….. UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM KWA VITENDO….**

**Prof Dr.rer.nat. Sospeter M Muhongo (MP)**
***(Officier, Ordre Palmes Academiques)***
***FGSAf, FAAS, MASSAf, FASI, FASSAf, FTAAS, FGIGE, FTWAS, HonRFCAGS, HonFGSA, HonFGS, CGeol, EurGeol***

***Masahihisho yamefanywa tarehe 20/12/2019***